

**MUUNDO WA KIRAI KITENZI KATIKA LUGHA YA KINDALI**

**DENIS KIBONA**

**TASINIFU HII IMEWASILISHWA KWA AJILI YA KUKAMILISHA  
SEHEMU YA MASHARTI TA KUTUNUKIWA SHAHADA YA UZAMILI YA  
KISWAHILI (ISIMU) KATIKA IDARA YA LUGHA NA TAALUMA ZA  
FASIHI YA CHUO KIKUU HURIA CHA TANZANIA**

**2022**

## **UTHIBITISHO**

Aliyetia saini hapa chini anathibitisha kwamba ameisoma tasnifu hii yenye anuani “**Muundo wa Kirai Kitenzi katika Lugha ya Kindali**”, na anapendekeza ikubaliwe na Chuo Kikuu Huria cha Tanzania kwa ajili ya kukamilisha sehemu ya masharti ya kutunukiwa shahada ya uzamili ya Kiswahili katika Idara ya Lugha na Taaluma za Fasihi ya Chuo Kikuu Huria cha Tanzania

.....  
Dkt. Salma Hamad

(Msimamizi)

Tarehe: .....

**TAMKO**

Mimi, Denis Kibona nathibitisha kwamba tasnifu hii ni kazi yangu mwenyewe na haijawahi kuwasilishwa na wala haitawasilishwa katika chuo kikuu kingine kwa ajili ya mahitaji ya kutunukiwa shahada kama hii au nyingine yoyote.

Sahihi.....

Tarehe.....

**TABARUKU**

Kazi hii ninaitabaruku kwa mke wangu Esther Benard Mwasongwe na watoto wangu Eunice na Klara kwa mapenzi yao makubwa na ustahimilivu wa hali ya juu kwangu wakati wote wa kufanya utafiti huu.

## SHUKRANI

Utafiti huu umefanyika kwa kuwashirikisha watu mbalimbali wa ndani na nje ya wilaya ya Ileje, hivyo wote wale ambao walifanikisha kukamilika kwa utafiti huu wanapewa shukrani za dhati kabisa. Kwanza, napenda kutoa shukrani maalumu na za kipekee kwa msimamizi wangu Dkt.Salma Hamad ambaye alifuatilia utafiti huu kwa makini hatua baada ya hatua na kunielekeza pale nilipokuwa nimekwama. Mwongozo na ushauri alionipa wakati wote wakufanya utafiti huu umenifungua macho katika masuala ya kiusomi kwa njia ya kipekee. Hakika mwongozo na ushauri wake ndio ulifanikisha kukamilika kwa utafiti huu.

Pili, shukrani zangu napenda kuzitoa kwa wahadhiri wangu wote wa Chuo Kikuu Huria cha Tanzania ambao walifanikisha vizuri masomo yangu pamoja na wanafunzi wenzangu kwa ushirikiano walionipa tangu kuanza kwa masomo hadi kumaliza.

Vilevile namshukuru Mkuu wa shule ya sekondari Kigonsera Bw.Ponsiano Ngungulu kwa kuniruhusu kuendelea na masomo hasa kwa kuandaa ratiba ya kazi iliyoniruhusu kuhudhuria masomo bila kutatiza shughuli zangu za kazi.

Mwisho, ninamshukuru MUNGU muweza wa yote, kwa ulinzi na majaliwa yake kuniwezesha kusoma katika hali zilizokuwa ngumu, kuniongoza, kunihifadhi na zaidi kuniwezesha kukamilisha utafiti huu.

**VIFUPISHO**

N	Nomino
T	Kitenzi
W	Kiwakilishi
V	Kivumishi
E	Kielezi
H	Kihusishi
KN	Kirai nomino
KT	Kirai kitenzi
KV	Kirai kivumishi
KE	Kirai elezi
KH	Kirai husishi
S	Sentensi
Š	Kishazi kijalizi

**IKISIRI**

Utafiti huu unahusiana na muundo wa kirai kitenzi cha lugha ya Kindali ambao umefanyika katika wilaya ya Ileje ambapo ndio eneo halisi la wazungumzaji wa lugha hiyo. Lengo kuu la utafiti huu ni kuchunguza muundo wa kirai kitenzi katika lugha ya Kindali. Malengo mahususi ni kubainisha vipashio vya muundo wa kirai kitenzi katika lugha ya Kindali, kuelezea mpangilio wa vipashio vya muundo wa kirai kitenzi katika lugha ya Kindali, na kujadili dhima za kisarufi za kirai kitenzi cha lugha ya Kindali. Utafiti huu umehusisha wazee kuanzia miaka hamsini (50) na sabini (70), ambao ni wakazi wa kata ya Kafule. Data za utafiti huu zilipatikana kutokana na hojaji zilizotayarishwa ambazo zilikuwa na maswali tofauti yaliyokuwa yanahusiana na kirai kitenzi cha lugha ya Kindali. Watoa taarifa hao walitakiwa kujibu maswali yote ili data sahihi ziweze kupatikana. Matokeo ya utafiti huu yanaonesha kuwa muundo wa kirai kitenzi cha lugha ya Kindali unavipashio vinavyoandamana navyo, vipashio hivyo ni kama vile nomino, kitenzi kisaidizi, kitenzi kikuu, kivumishi, kielezi na sentensi. Utafiti huu umependekeza kuwa ufanyike utafiti ambao unahusu kirai kihusishi cha lugha ya Kindali kwa kutumia nadharia ya x- baa.

**Maneno Makuu:** *Kitenzi, Kirai, Sentensi*

## YALIYOMO

UTHIBITISHO .....	ii
TAMKO .....	iii
TABARUKU .....	iv
SHUKRANI .....	v
VIFUPISHO .....	vi
IKISIRI .....	vii
YALIYOMO .....	viii
ORODHA YA MAJEDWALI .....	xii

### **SURA YA KWANZA: UTANGULIZI.....1**

1.1	Utangulizi wa Sura ya Kwanza.....	1
1.2	Usuli wa Mada .....	1
1.3	Tatizo la Utafiti .....	2
1.4	Malengo ya Utafiti .....	2
1.4.1	Lengo Kuu .....	3
1.4.2	Malengo Mahususi .....	3
1.5	Maswali ya Utafiti.....	3
1.6	Umuhimu wa Utafiti .....	3
1.7	Mipaka ya Utafiti .....	4

### **SURA YA PILI: MAPITIO YA KAZI TANGULIZI NA KIUNZI CHA**

	<b>NADHARIA .....</b>	<b>5</b>
2.1	Utangulizi.....	5
2.2	Fasili ya dhana .....	5



2.2.1	Vitenzi.....	5
2.2.2	Kirai .....	6
2.2.3	Dhana ya kirai kitenzi .....	7
2.2.4	Muundo wa kirai kitenzi katika Kiswahili sanifu .....	7
2.2.5	Dhima za Kisarufi za Kirai Kitenzi.....	12
2.3	Tafiti Tangulizi Kuhusu Lugha ya Kindali .....	13
2.4	Tafiti Tangulizi kuhusu kirai kitenzi katika lugha za Kibantu.....	16
2.5	Pengo la maarifa.....	18
2.6	Kiunzi cha nadharia .....	19
2.6.1	Nadharia ya Sarufi Miundo virai .....	19
2.6.2	Nadharia ya x-baa .....	20
2.7	Hitimisho.....	24
<b>SURA YA TATU: MBINU ZA UTAFITI.....</b>		<b>25</b>
3.1	Utangulizi.....	25
3.2	Eneo la utafiti .....	25
3.3	Mbinu za ukusanyaji data .....	25
3.3.1	Mbinu ya hojaji .....	26
3.4	Vifaa vya kukusanyia data .....	27
3.5	Sampuli .....	27
3.6	Usampulishaji .....	28
3.7	Mkabala wa uchambuzi wa data za utafiti .....	29
3.8	Maadili ya utafiti.....	29
3.9	Changamoto zilizojitokeza wakati wa ukusanyaji wa data.....	30

3.10	Hitimisho.....	30
<b>SURA YA NNE: UWASILISHAJI NA UCHAMBUZI WA DATA.....</b>		<b>31</b>
4.1	Utangulizi.....	31
4.2	Muundo wa kirai kitenzi katika lugha ya Kindali.....	31
4.2.1	Kitenzi peke yake (KT → T).....	31
4.2.2	Kitenzi na nomino moja (KT → T+N).....	32
4.2.3	Kitenzi na nomino mbili (KT → T+N+N).....	33
4.2.4	Kitenzi na kitenzi (KT → TS+T).....	34
4.2.5	Kitenzi na nomino na kitenzi (KT → T+N+T).....	36
4.2.6	Kitenzi na kivumishi (KT → T+V).....	37
4.2.7	Kitenzi na kielezi (kirai kielezi) (KT → T+KE).....	38
4.2.9	Kitenzi na sentensi (KT → T+S).....	40
4.3	Kuchanganua mpangilio wa vipengele katika kirai kitenzi.....	42
4.3.1	Kirai kitenzi cha kitenzi peke yake.....	42
4.3.2	Kirai kitenzi cha kitenzi na nomino moja.....	43
4.3.3	Kirai kitenzi cha kitenzi na nomino mbili.....	45
4.3.4	Kirai kitenzi cha kitenzi na kitenzi.....	46
4.3.5	Kirai kitenzi cha kitenzi na nomino na kitenzi.....	48
4.3.6	Kirai kitenzi cha kitenzi na kivumishi.....	49
4.3.7	Kirai kitenzi cha kitenzi na kielezi.....	51
4.3.8	Kirai kitenzi cha kitenzi na kirai kihushi.....	52
4.3.9	Kirai kitenzi cha kitenzi na sentensi.....	54
4.4	Kubainisha dhima za kisarufi za kirai kitenzi katika lugha ya Kindali.....	56

4.4.1	Kirai kitenzi hutumika kama kivumishi cha kirai nomino.....	56
4.4.2	Kirai kitenzi hufanya kazi kama kijalizo cha kirai nomino. ....	57
4.4	Hitimisho.....	59

## **SURA YA TANO: MUHTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO YA**

	<b>UTAFITI .....</b>	<b>60</b>
5.1	Utangulizi.....	60
5.2	Muhtasari wa Utafiti .....	60
5.3	Muhtasari wa Matokeo ya Utafiti .....	61
5.4	Mapendekezo ya Utafiti.....	62
5.5	Hitimisho.....	62
	<b>MAREJELEO .....</b>	<b>63</b>
	<b>VIAMBATANISHO .....</b>	<b>67</b>

## ORODHA YA MAJEDWALI

Jedwali Na.4.1	Kirai kitenzi cha kitenzi peke yake. ....	42
Jedwali Na. 4.2	kirai kitenzi cha kitenzi pekee. ....	42
Jedwali Na.4.3	kirai kitenzi cha kitenzi na nomino moja .....	43
Jedwali Na. 4.4	kirai kitenzi cha kitenzi na nomino moja .....	43
Jedwali Na. 4.5	kirai kitenzi cha kitenzi na nomino moja .....	44
Jedwali Na 4.6	kirai kitenzi cha kitenzi na nomino mbili .....	45
Jedwali Na. 4.7	kirai kitenzi cha kitenzi na nomino mbili .....	45
Jedwali Na.4.8	kirai kitenzi cha kitenzi na kitenzi .....	46
Jedwali Na. 4.9	kirai kitenzi cha kitenzi na kitenzi .....	47
Jedwali Na. 4.10	kirai kitenzi cha kitenzi na kitenzi .....	47
Jedwali Na. 4.11	kirai kitenzi cha kitenzi na nomino na kitenzi .....	48
Jedwali Na. 4.12	kirai kitenzi cha kitenzi na nomino na kitenzi .....	48
Jedwali Na.4.13	kirai kitenzi cha kitenzi na kivumishi .....	49
Jedwali Na.4.14	kirai kitenzi cha kitenzi na kivumishi .....	50
Jedwali Na.4.15	kirai kitenzi cha kitenzi na kielezi .....	51
Jedwali Na.4.16	kirai kitenzi cha kitenzi na kirai kihusishi .....	52
Jedwali Na.4.17	kirai kitenzi cha kitenzi na kirai kihusishi .....	53
Jedwali Na.4.18	kirai kitenzi cha kitenzi na sentensi .....	54
Jedwali Na.4.19	kirai kitenzi cha kitenzi na sentensi .....	54

## **SURA YA KWANZA**

### **UTANGULIZI**

#### **1.1 Utangulizi wa Sura ya Kwanza**

Utafiti huu unahusu uchanganuzi wa muundo wa kirai kitenzi (KT) katika lugha ya Kindali kwa kutumia nadharia ya Sarufi Miundo Virai. Mtafiti alibainisha virai vitenzi vinavyojitokeza katika lugha ya Kindali. Sura hii ya kwanza imejitokeza katika sehemu saba (7). Sehemu ya kwanza imeanza kwa utangulizi, sehemu ya pili imeelezea usuli wa mada, sehemu ya tatu imeelezea tatizo la utafiti, sehemu ya nne imeelezea malengo ya utafiti, sehemu ya tano imeelezea maswali ya utafiti, sehemu ya sita imeelezea umuhimu wa utafiti na sehemu ya saba imeelezea mipaka ya utafiti.

#### **1.2 Usuli wa Mada**

Kindali au Chindali ni miongoni mwa lugha za Kibantu inayozungumzwa nchini Tanzania. Wazungumzaji wa lugha hii ni Wandali wanaopatikana wilaya ya Ileje katika mkoa wa Mbeya kwasasa Songwe. Wilaya ya Ileje ilikuwa na wazungumzaji 124,451 (Sensa ya watu 2012). Pia lugha ya Kindali inazungumzwa Kasikazini mwa Malawi na ipo katika kundi la M21 (Botne, 1998). Kindali (au Chindali) ni lugha ya kibantu nchini Tanzania inayozungumzwa na Wandali wanaopatikana kusini magharibi mwa mkoa wa Mbeya nchini Tanzania na kasikazini mwa wilaya ya Chitipa nchini Malawi, ambapo nchini Malawi kuna wazungumzaji karibia 70,000 na wazungumzaji 150,000 nchini Tanzania (Botney na Schafer, 2008). Wilaya ya Ileje upande wa kasikazini inapakana na wilaya ya Mbeya vijijini na Rungwe, Mashariki inapakana na wilaya ya Kyela na upande wa Kusini inapakana na nchi ya Malawi.

Lugha ya kindali ni mojawapo ya lugha za Kibantu ambayo imefanyiwa tafiti kadhaa. Miongoni mwa tafiti hizo ni ule wa Swilla (1998) unaohusu uchunguzi wa njeo katika lugha ya Chindali. Mwingine ni wa Botne (1998) ambaye alifanya utafiti juu ya masharti ya kiarudhi ya ufupishaji wa Irabu katika Chindali. Swilla (2000) alifanya uchunguzi kuhusiana na majina ya Chindali. Pia Swilla (2005) alishughulikia mienendo ya udumishaji wa lugha ya Chindali katika wilaya ya Mbozi, Tanzania. Masebo (2007) alifanya utafiti kuhusiana na upanuzi (mnyambuliko) wa vitenzi katika lugha ya Chindali. Botne na Schafer (2008) walishughulikia kamusi ya Chindali – Kiingereza katika lugha ya Chindali. Mshani (2014) alifanya uchunguzi katika maumbo na dhima ya uradidi wa vitenzi vya Chindali. Vilevile Kibona (2016) alifanya utafiti juu ya uchanganuzi wa kirai nomino katika lugha ya Kindali. Tafiti hizi zimefafanua vipengele muhimu vya kiisimu katika lugha ya Kindali. Hata hivyo, bado kuna vipengele vya kiisimu havijafanyiwa utafiti, muundo wa kirai kitenzi ni mojawapo ya vipengele hivyo. Utafiti huu umekifanyia kazi kipengele hicho.

### **1.3 Tatizo la Utafiti**

Ingawa tafiti kadhaa zimefanywa katika lugha ya Kindali kwa kuangalia vipengele tofauti vya kiisimu, kwa uelewa wa mtafiti kipengele cha muundo wa kirai kitenzi cha lugha ya Kindali bado hakijafanyiwa utafiti, kwa hiyo utafiti huu ulishughulikia kipengele hiki cha muundo wa kirai kitenzi katika lugha ya Kindali.

### **1.4 Malengo ya Utafiti**

Utafiti huu una lengo kuu na malengo mahususi matatu.

### **1.4.1 Lengo Kuu**

Lengo kuu la utafiti huu ni kuchunguza muundo wa kirai kitenzi katika lugha ya Kindali. Katika kufikia lengo hili, utafiti huu umeongozwa na malengo mahususi yafuatayo:

### **1.4.2 Malengo Mahususi**

- i) Kubainisha vipashio vya muundo wa kirai kitenzi katika lugha ya Kindali
- ii) Kuelezea mpangilio wa vipashio vinavyounda kirai kitenzi katika lugha ya Kindali.
- iii) Iii. Kujadili dhima za kisarufi za kirai kitenzi cha lugha ya Kindali.

### **1.5 Maswali ya Utafiti**

- i) Muundo wa kirai kitenzi katika lugha ya kindali una vipashio vipi?
- ii) Vipashio vinavyounda kirai kitenzi katika lugha ya Kindali vipo katika mpangilio upi?
- iii) Kirai kitenzi katika lugha ya Kindali kina dhima gani kisarufi?

### **1.6 Umuhimu wa Utafiti**

Mtafiti yeyote wa kitaaluma huwa na shauku ya kuongeza maarifa yenye kuleta tofauti na kuongeza ufanisi katika uwanja anaoutafiti. Utafiti huu kuhusu muundo wa kirai kitenzi katika lugha ya Kindali utakuwa na umuhimu ufuatao:

Utafiti huu utatoa mchango mkubwa katika taaluma ya Sintaksia katika uchanganuzi wa kirai kitenzi (KT) cha lugha ya Kindali. Nidhahiri kwamba utafiti huu utatoa mchango wa kutosha kwa wanaisimu kuhusiana na uchanganuzi wa virai vya lugha nyingine za Kibantu.

Aidha utafiti huu unatarajiwa kuwa na faida kubwa kwa kujaza pengo ambalo lipo kwa upande wa lugha ya Kindali kwa kuongeza maarifa katika kipengele hiki cha kiisimu.

Matokeo ya kazi hii, pia yatasaidia kuwa marejeleo kwa watafiti wengine ambao wanakusudia kutafiti lugha nyingine za Kibantu.

### **1.7 Mipaka ya Utafiti**

Utafiti huu ulijikita katika kuchanganua muundo wa kirai kitenzi katika lugha ya Kindali ambayo huzungumzwa katika eneo la wilaya ya Ileje. Aidha utafiti huu ulijikita katika kubainisha vipashio vinavyounda kirai kitenzi cha lugha ya Kindali pamoja na kuchanganua mpangilio wa vipashio vinavyounda kirai kitenzi hicho, pia kubainisha dhima za kisarufi za kirai kitenzi katika lugha ya Kindali.



## SURA YA PILI

### MAPITIO YA KAZI TANGULIZI NA KIUNZI CHA NADHARIA

#### 2.1 Utangulizi

Sura hii ya pili inahusu mapitio ya kazi tangulizi pamoja na kiunzi cha nadharia. Kwanza, mtafiti ametoa fasili ya dhana mbalimbali ambazo zimetumika katika utafiti huu. Dhana hizo ni kitenzi, kirai na kirai kitenzi. Aidha katika sura hii mtafiti aliangalia kazi tangulizi kuhusiana na lugha ya Kindali, muundo wa kirai kitenzi katika lugha za kibantu, kiunzi cha nadharia na amemaliza kwa hitimisho.

#### 2.2 Fasili ya dhana

Sehemu hii imefafanua dhana mbalimbali kama ifuatavyo:

##### 2.2.1 Vitenzi

Vitenzi ni moja wapo ya kategoria katika sintaksia inayounda sentensi katika lugha. Wataalamu mbalimbali wameeleza kuhusu kitenzi;

Kihore na wenzake (2003) wanafafanua kuwa kitenzi ni aina ya neno linalotoa taarifa juu ya tendo linalofanyika au linalotendwa na kiumbe au kitu. Wanaendelea kueleza kuwa kuna aina kuu tatu ya vitenzi ambavyo ni kitenzi kikuu mfano Baba **anakula** ugali, kitenzi kisaidizi, mfano; Baba **alikuwa** anakula ugali na kitenzi kishirikishi, mfano; Juma **ni** mwanafunzi mzuri. Maneno yaliyokolezwa wino ni aina ya vitenzi hivyo. Mgullu (2012) anasema vitenzi ni aina ya maneno ambayo hutumika kama sehemu muhimu sana ya kiarifu cha sentensi na ambavyo hueleza jambo fulani linalohusiana na kiima. Anaendelea kueleza kwamba katika lugha ya Kiswahili vitenzi ni maneno pekee ambayo lazima yawepo katika sentensi ndipo sentensi iweze kuwa sentensi.

### 2.2.2 Kirai

Massamba na wenzake (2001), Kamusi ya Longhorn (2011) na Riro (2012) wanaielezea dhana ya kirai kuwa ni kipashio cha kisarufi kinachoundwa na neno moja au zaidi na hakina mwingiliano wa kimuundo wa kiima na kiarifu.

Radford (2004) anadai kuwa kila kirai kina kichwa kinachoamua sifa za kirai chote. Kwa mfano; **Mwanafunzi** wa hisabati. **Mwanafunzi** (umoja) ni kichwa cha kirai na ndicho kinachoamua sifa ya kirai husika. Kirai huainishwa kimuundo kulingana na neno kuu/kichwa cha kirai husika. Hivyo, kirai ambacho neno lake kuu ni nomino au kiwakilishi huitwa kirai nomino, Kwamfano; *mtoto* huyu. Hapa neno kuu ni mtoto, ndipo kirai hicho kikaitwa kirai nomino. Kwamantiki hii aina fulani ya neno kuu huwa msingi wa uundaji wa virai. Neno hilo kuu linaweza kuwa nomino, kitenzi, kivumishi, kielezi, kiunganishi au kihusishi. Kwamsingi huu kuna aina zifuatazo za virai;

- a) Virai nomino
- b) Virai vitenzi
- c) Virai vivumishi
- d) Virai vielezi
- e) Virai vihusishi

Matei (2008) kirai ni fungu la maneno ambalo hufanya kazi kama neno moja au huwa na uamilifu sawa. Hivyo kirai ni fungu la maneno ambalo huundwa na neno moja au zaidi.

Barongo na wenzake (2019) wanaeleza kuwa kirai ni aina ya tungo yenye neno moja au zaidi ambayo uhusiano wake umekitwa katika neno kuu. Neno kuu katika kirai

hutokana na aina za maneno. Aina hizo za maneno zinaweza kusimama peke yake kama kirai au kuandamana na maneno mengine kwa kuzingatia uhusiano maalumu baina ya maneno hayo na neno kuu.

Katika utafiti huu mtafiti amechunguza muundo wa kirai kitenzi katika lugha ya Kindali.

### **2.2.3 Dhana ya kirai kitenzi**

Dhana ya kirai kitenzi kama kipashio cha kiisimu imejadiliwa sana na wataalamu waliochunguza lugha mbalimbali.

Massamba na wenzake (2001) wanasema kuwa kirai kitenzi ni kirai ambacho kimekitwa katika kitenzi au katika mahusiano ya kitenzi na neno au mafungu mengine ya maneno. Hii inamaana kuwa neno kuu katika aina hii ya kirai huwa ni kitenzi. Riro (2012) anaeleza kuwa kirai kitenzi huundwa kwa kitenzi na maneno mengine yanayohusiana na kitenzi hicho. Neno kuu katika kirai hiki ni kitenzi chenyewe.

Masebo na Nyangwine (2016) wamefasili kirai kitenzi kuwa ni kundi ambalo hufanya kazi pamoja kama kitenzi. Neno lake kuu huwa kitenzi. Kutokana na uchambuzi wa wataalamu hawa, dhana ya jumla inayopatikana kuhusu maana ya kirai kitenzi ni kuwa kirai kitenzi ni kirai ambacho neno lake kuu ni kitenzi na huweza kusimama peke yake au kuambatana na maneno mengine.

### **2.2.4 Muundo wa kirai kitenzi katika Kiswahili sanifu**

Massamba na wenzake (2001) wao wanasema kirai kitenzi kina miundo saba kama ifuatayo:

a) Kitenzi peke yake. Kwafano:

Amekufa

walipona

b) Kitenzi na nomino moja kama katika:

Amempiga Juma.

Amempiga=kitenzi

Juma= nomino

Wamekata mti

Wamekata =kitenzi

Mti = nomino

c) Kitenzi na nomino mbili kama katika:

Wanampigia Juma kelele

Wanampigia = kitenzi

Juma = nomino<sub>1</sub>

Kelele = nomino<sub>2</sub>

Tumemnyima mwanafunzi daftari

Tumemnyima = kitenzi

Mwanafunzi = nomino<sub>1</sub>

Daftari = nomino<sub>2</sub>

d) Kitenzi na kitenzi kama katika:

Tunataka kulala

Tunataka = kitenzi

Kulala = kitenzi

Ameamua kurudi

Ameamua = kitenzi

Kurudi = kitenzi

e) Kitenzi nomino na kitenzi kama katika:

Anamfundisha mtoto kusoma

Anamfundisha = kitenzi

Mtoto = nomino

Kusoma = kitenzi

Tumemlazimisha Juma kula

Tumemlazimisha= kitenzi

Juma=nomino

Kula=kitenzi

f) Kitenzi (na kwamba/kuwa) na sentensi kama katika:

**Amesema (kwamba) atarudi kesho**

**Amelalamika (kwamba) amelazimishwa kwenda shule**

g) Kitenzi na nomino (na kwamba/kuwa) na sentensi kama katika:

**Amemwambia Juma(kwamba)arudi kesho**

**Amemwagiza mama (kwamba) aniletee chumvi**

Kwa upande mwingine Masebo na Nyangwine (2016) wao wameainisha miundo kumi na moja ya kirai kitenzi miundo mitano inafanana na ile ya Massamba na wenzake (2001) lakini miundo miwili aliyoainisha Massamba(ameshatajwa) yaani muundo wa sita na saba unatofautiana kabisa na miundo yote iliyoainishwa na Masebo na Nyangwine (2016) kama ifuatavyo:

- i. Kitenzi kikuu peke yake mfano:  
Mwizi **ameshikwa**  
“Ameshikwa” ni kitenzi kikuu
- ii. Vitenzi visaidizi na vitenzi vikuu.mfano:  
Juma **alikuwa anasoma**  
“Alikuwa” ni kitenzi kisaidizi na “anasoma” ni kitenzi kikuu
- iii. Kitenzi na kirai nomino.mfano:  
Frank **ameandika barua ndefu mno**  
“Ameandika”ni kitenzi(T) na “barua ndefu mno”ni kirai nomino
- iv. Kitenzi kikuu na kielezi. Mfano:  
Maria **anasoma polepole.**  
“Anasoma” ni kitenzi kikuu (T) na “polepole” ni kielezi.
- v. Kitenzi kikuu na kishazi tegemezi kielezi. Mfano:  
Mtoto **alilia alipopigwa**  
“Analia” kitenzi kikuu (T) na “alipopigwa” kishazi tegemezi kielezi.
- vi. Kitenzi kikuu na kirai kihusishi. Mfano:  
Damasi **amenijibu kwa hasira**  
“Amenijibu” kitenzi kikuu na “kwa hasira” ni kirai kihusishi.
- vii. Kitenzi kishirikishi na kielezi. Mfano:  
Mwalimu **yumo darasani**  
“Yumo” ni kitenzi kishirikishi na “darasani” ni kielezi.
- viii. Kitenzi kishirikishi na kivumishi. Mfano:  
Roza **ni mzuri**  
“Ni” ni kitenzi kishirikishi na “mzuri” ni kivumishi.

ix. Kitenzi kishirikishi na nomino. Mfano:

Juliana **ni mototo**

“Ni” ni kitenzi kishirikishi na “mtoto” ni nomino.

x. Kitenzi kishirikishi na kirai nomino. Mfano:

Huu **ni mpango mzuri**

“Ni” ni kitenzi kishirikishi na “mpango mzuri” ni kirai nomino.

xi. Vitenzi vikuu sambamba. Mfano

Wanafunzi **wanacheza wakicheka**

“Wanacheza” na “wakicheka” ni vitenzi vikuu sambamba

Maneno yaliyo kolezwa wino ni kirai kitenzi.

Riro (2012) yeye ameelezea miundo sita ya kirai kitenzi ambapo miundo mitano inafana na ile ya Massamba (2001) lakini miundo miwili inatofautiana yaani muundo wa sita na wa saba wa Massamba (2001) haujaainishwa kabisa na Riro (2012) lakini miundo yote sita iliyoainishwa na Riro (ameshatajwa) imeainishwa pia na Masebo na Nyangwine (2016) katika ile miundo kumi na moja, miundo iliyoainishwa na Riro (ameshatajwa) ni kama ifuatavyo:

i. Kitenzi kimoja

Mwalimu *amefika*

ii. Kitenzi na nomino moja

*Wamenunua viatu*

iii. Kitenzi na nomino mbili

Rehema *amempatia mototo kalamu*

iv. Kitenzi na kitenzi

*Anapenda kucheza*

v. Kitenzi na kielezi

*Mtoto amelia mno*

vi. Kitenzi, nomino na kitenzi

*Tulimwomba mwalimu ahubiri.*

Maneno yaliyokwenye maandishi ya mlalo ni kirai kitenzi.

Kazi za wataalamu hawa zimemsaidia mtafiti katika kubainisha muundo wa kirai kitenzi katika lugha ya Kindali.

### **2.2.5 Dhima za Kisarufi za Kirai Kitenzi**

Sarufi ni mfumo wa kanuni za lugha zinazomwezesha mzungumzaji kutunga sentensi nyingi sahihi na zenye kukubaliwa na wazawa wa lugha (Mdee1999).

Dhima za kisarufi za kirai kitenzi ni majukumu ya kisarufi ambayo kirai kitenzi hutekeleza katika kutunga sentensi. John na Mduda (2012) wanaeleza kuwa kirai kitenzi kina dhima zifuatazo:

a) Kubainisha kitendo kilicho tendeka, kinachotendeka au kitakacho tendeka.

Kwamfano: Watoto *wanasoma* (kitendo kinachotendeka)

Dola *alikuwa anakutafuta* (kitendo kilicho tendeka)

Mimi *nitakuwa nimepumzika* (kitendo kitakachotendeka)

b) Kuonesha hali ya tendo, yaani hali ya kuendelea, utimilifu au

mazoea. Kwamfano:

Katibu *anaandika ripoti.* (hali ya kuendelea)

Ukija *nitakuwa nimesharudi.* (hali ya wakati ujao utimilifu)

Yeye *huwa anasahau.* ( hali ya mazoea)



c) Kuonesha iwapo kiima kinatenda au kinaathiriwa na tendo. Kwamfano:

Chambo *alikuwa anakutafuta* (kiima “Chambo” kinatenda)

Chambo *alikuwa anatafutwa* (hapa kiima “Chambo” kinaathiriwa na tendo)

Kazi za watalaamu hawa zimemsaidia mtafiti kuweza kubainisha dhima za kisarufi za kirai kitenzi katika lugha ya Kindali

### **2.3 Tafiti Tangulizi Kuhusu Lugha ya Kindali**

Kama ilivyoelezwa kwenye sura ya kwanza, ijapo tafiti nyingi zimefanywa kuhusu lugha ya Kindali lakini matokeo ya tafiti hizo yametoa maelezo machache ambayo yanamchango katika ulimwengu wa isimu na lugha kwa ujumla. Baadhi ya waliofanya utafiti kuhusu Kindali ni:

Botne (1998) alifanya utafiti juu ya masharti ya kiarudhi ya ufupishaji wa irabu katika Chindali. Katika uchunguzi wake alibaini kuwa Katika lugha ya Chindali kuna nomino ambazo shina lake linaweza kupunguzwa na ukapata nomino nyingine mfano Un’oko (mama)-u: n’okokulu (shangazi): Pia, alibaini kuwa kuna aina kumi na nane za kweli katika Chindali. Swilla (2000) alifanya uchunguzi katika majina ya Chindali. katika utafiti wake aligundua kuwa katika jumuiya ya wanaozungumza Chindali angalau huwa na aina tano za majina ambayo ni: majina ya utotoni, majina ya kusifu, majina binafsi, majina ya ukoo, na majina ya sifa za ukoo. Swilla (ameshatajwa) Anaendelea kuelezea kuwa mababu ndio wanajukumu kubwa la kuchagua na kutoa majina ya utotoni. Majina ya ukoo yamewekwa ambayo hupitishwa kutoka kizazi hadi kizazi kupitia watoto wa kiume. Wazazi huwachagua watoto majina yao lakini baadae hao watoto wanaweza kujichagua majina yao ya maisha.

Swilla (2002) alichunguza uhai wa Chindali miongoni mwa wazungumzaji wanao hama kutoka Ileje kwenda Mbozi Kusini-Magharibi mwa Tanzania. Uchunguzi wake ulibaini kuwa kuna viashiria vya awali vya uhamishaji wa maneno kutoka kwenye Chindali kwenda kwenye Kiswahili. Vilevile Swila (ameshatajwa) alibaini kuwa watu wanaozungumza lugha moja (Chindali) ni wachache sana na wanaozungumza lugha mbili ya Chindali na Kiswahili unaongezeka kwa kasi ambapo wanaazima maneno ya Kiswahili na kuyatumia katika Chindali. Mathalani, Mulumbu (neni la awali) ndanda (neni lililoazimwa kutoka kwenye Kiswahili dada). Pia kuchanganya lugha ya Kiswahili na Chindali ni kawaida kwa sasa. Kwamfano: Ujuma akukinda sana (chindali) Juma anakimbia sana (Kiswahili). Na matumizi ya Kiswahili yanaongezeka katika familia na kwa jamii.

Pamoja na hayo, Swilla (2005) alishughulikia mienendo ya udumishaji wa lugha ya Chindali katika wilaya ya Mbozi, Tanzania katika utafiti huo alibaini kuwa kuna udumishaji wa lugha. Swila(ameshatajwa) anaeleza kwamba vitu vinavyosababisha udumishaji wa lugha ya Chindali inayozungumzwa wilaya ya Mbozi ni tamaa ya kutunza na kujitofautisha na makundi mengine katika eneo jipya na fahari katika utamaduni, uongaji wa lugha moja, Chindali kama lugha ya familia na jamii ya Wandali, kiwango kidogo cha elimu rasmi na kuendelea kuwasiliana na Wandali. Masebo (2007) alifanya utafiti kuhusiana na upanuzi (mnyambuliko) wa vitenzi katika lugha ya Chindali alibaini kuwa lugha ya Chindali inafanana sana na lugha nyingine za kibantu katika nyanja zake mbalimbali ukiwemo mnyambuliko wa vitenzi. Masebo (ameshatajwa) anaendelea kuelezea kuwa viambishi mbalimbali katika lugha ya Chindali huongezeka au hupungua kutokana na kutofautiana kwa

vitenzi na viambishi vingi tamati ambavyo husababisha maumbo changamano ya kimofolojia, utaratibu ambao ni thabiti. Mpangilio huo unaendana na uhamishaji kisintaksia. Katika ujenzi wa vitenzi, viambishi tamati huonesha kwamba uundaji wa kileksia ya kimatamshi na mchakato unaohusika kimsingi ni mofosintaksia. Botne na Schafer (2008) walishughulikia kamusi ya Chindali - Kiingereza. Katika utafiti wao walibaini kuwa kuna aina mbalimbali za Chindali kinachozungumzwa kasikazini mwa Malawi ukiondoa Kisukwa. Mshani (2014) alifanya utafiti kuhusiana na maumbo na dhima ya uradidi wa vitenzi katika lugha ya Chindali. Katika utafiti wake alibaini kuwa kuna aina mbili za uradidi katika lugha ya Chindali ambao ni uradidi kamili unaohusu urudiaji wa shina au neno lote na uradidi nusu ambao ni urudiaji wa sehemu tu ya neno au shina na umeonekana katika vitenzi vinavyoonesha njeo pamoja na vitenzi visoukomo vinavyoandamana na kiambishi kisoukomo na aina nyingine za viambishi awali vinavyojitokeza kabla ya mzizi wa kitenzi. Uradidi nusu katika Chindali unahusu unakili wa mzizi wa kitenzi na viambishi tamati. Pia anaendelea kuelezea kuwa viradidiwa katika lugha ya Chindali hutokea kabla au baada ya mzizi au shina la kitenzi kwa kunakili kuanzia upande wa kushoto kuelekea upande wa kulia wa shina au mzizi wa kitenzi. Aidha anabainisha dhima mbalimbali za uradidi katika lugha ya Chindali kama vile kusisitiza jambo, kujirudia kwa jambo, udhofishaji wa maana, hali ya mazoea na dhima ya kuendelea kwa jambo.

Mtafiti mwingine ni Kibona (2016) aliyefanya uchunguzi juu ya uchanganuzi wa kirai nomino katika lugha ya Kindali na kubainisha miundo sita ya kirai nomino cha lugha ya Kindali. Katika uchunguzi wake aliainisha jinsi vijalizo vinavyojipanga kuunda kirai nomino katika lugha ya Kindali. Mfano N+Ditamina: Umwana jhula-

Mtoto yule. Anaendelea kuelezea kuwa katika lugha ya Kindali hakuna vibainishi bali kuna viambishi awali ambavyo hutokea katika kirai nomino, Mfano: U-mkolo U-mwolo (mwanamke mvivu)

Tafiti tangulizi hizo katika lugha ya Kindali zimesaidia kujua pengo la utafiti kwasababu hakukuwa na utafiti wowote uliofanyika kuhusu kirai kitenzi cha lugha ya Kindali.

#### **2.4 Tafiti Tangulizi kuhusu kirai kitenzi katika lugha za Kibantu**

Tafiti mbalimbali kuhusu kirai kitenzi cha lugha za Kibantu zimekwisha fanywa katika lugha mbalimbali kaama ifuatavyo:

Haji (2018) alifanya utafiti katika lahaja ya Kitumbatu, ambapo alibaini kuwa kirai kitenzi cha lahaja ya Kitumbatu kina vipashio vinavyoandamana navyo. Vipashio hivyo ni kama vile nomino, kitenzi kisaidizi, kijalizi tegemezi na sentensi, kihusishi na kielezi. Pia Haji (ameshatajwa) anaendelea kueleza kuwa katika lahaja ya Kitumbatu kuna vitenzi ambavyo lazima vifuatwe na nomino moja au mbili na vitenzi vingine haviwezi kufuatwa na nomino moja au mbili katika ukamilifu wake. Mfano; Kagere simu (Kitumbatu)-Amepoteza simu (Kiswahili). Katika mfano huo, kirai kitenzi kinaundwa na kitenzi (kagere) na nomino moja (simu). Pia, katika Kitumbatu kuna kitenzi ambacho hakiwezi kufuatwa na nomino moja au mbili. Mfano; Twantaka kulya (Kitumbatu) -Tunataka kula (Kiswahili). Hivyo, kwa mujibu wa maelezo ya Haji (2018) lahaja ya Kitumbatu ina miundo minane ya kirai kitenzi.

Mugisa (2011) alifanya uchunguzi wa muundo wa kisintaksia wa kirai kitenzi cha lugha ya Kihema. Kihema ni lugha ya kibantu inayozungumzwa Kasikazini-

Mashariki mwa jimbo la Ituri katika Jamhuri ya demokrasia ya Kongo. Katika uchunguzi wake Mugisa (2011) aligundua kuwa Kihema ni kama Kiingereza na lugha zingine za Kibantu, ambapo anaonesha kwamba virai vihusishi na kijalizo cha sentensi hutanguliwa na kitenzi. Mfano; Embwa e-ka-cumbi-ir-a(dog cooked food for the hen)- Mbwa alimpikia kuku chakula (Kiswahili). Neno “e-ka-cumbi-ir-a” katika mfano wa hapo juu ni kirai kitenzi cha lugha ya Kihema.

Habibu (2011) alibainisha miundo sita ya kirai kitenzi katika lugha ya Kisambaa. Katika utafiti wake amebainisha kuwa kuna vipashio vinavyo andamana na vitenzi hivyo. Mfano  $KT=T+KN+KN$  katika “Wavyazi waamzengea mwalimu nyumba” (wazazi wanamjengea mwalimu nyumba). Pamoja na hayo, Habibu (2011) alibaini kuwa muundo wa kirai kitenzi cha lugha ya Kisambaa unafanana sana na ule wa lugha ya Kiswahili.

Kanichi (2014) alifanya uchunguzi katika lugha ya Kinyakyusa mkoani Mbeya, ambapo aligundua kuwa kirai kitenzi cha Kinyakyusa kinaweza kuwa pekee na kufuatwa na kijalizo cha virai elezi ama virai vihusishi au nomino hasa katika vitenzi vishirikishi. Mfano; Ikibusu jali nkati-choo kilikuwa ndani. Katika sentensi hiyo” jali” ni kitenzi kishirikishi na “nkati “ ni kirai kielezi.

Ondondo (2015) naye alifanya uchunguzi wa muundo wa kirai kitenzi katika lahaja ya Kisa. Kisa ni lahaja ya lugha ya Luhya inayozungumzwa katika wilaya ya Khwisero Magharibi nchini Kenya. Katika uchunguzi wake alibaini kuwa kichwa (kitenzi) ni chalazima katika kirai kitenzi cha Kisa. Mathalani; Teekh-a muno bwaangu (pika haraka sana) kwa hiyo neno “teekh-a” ni kichwa cha kirai kitenzi

katika lugha ya Kisa. Pia katika uchunguzi wake Ondondo (2015) alibaini kuwa katika kirai kitenzi cha Kisa kina aina nne ya vijalizo ambavyo ni; kirai nomino, kirai kihusishi na kirai kielezi. Kwaujumla tunaona kuwa muundo wa kirai kitenzi katika lugha ya Kindali bado haujafanyiwa utafiti.

Kazi tangulizi zilizojadiliwa hapo juu zimemsaidia mtafiti kubaini muundo wa kirai kitenzi katika lugha mbalimbali za Kibantu. Aidha kutokana na kupitia kazi hizo ndipo mtafiti alipobaini pengo la utafiti baada ya kushindwa kupata kazi inayochambua muundo wa kirai kitenzi cha lugha ya Kindali. Hivyo kulikuwa na umuhimu wa kuangalia kirai kitenzi katika lugha ya Kindali.

## **2.5 Pengo la maarifa**

Kutokana na mapitio ya kazi tangulizi, tafiti mbalimbali zimekuwa zikifanyika juu ya muundo wa kirai kitenzi katika lugha za Kibantu.

Habibu (2011), alifanya utafiti juu ya muundo wa kirai kitenzi katika lugha ya Kisambaa. Mugisa (2011), alifanya utafiti juu ya “muundo wa kisintaksia wa kirai kitenzi cha lugha ya Kihema. Kanichi (2014), alifanya uchunguzi wa kirai kitenzi katika lugha ya Kinyakyusa. Ondondo (2015), alifanya uchunguzi wa muundo wa kirai kitenzi katika lugha ya Kisa. Vilevile, Haji (2018), alifanya utafiti katika lahaja ya Kitumbatu.

Kwa upeo wa ufahamu wa mtafiti hakuna mtafiti aliyewahi kujishughulisha na uchunguzi wa kirai kitenzi katika lugha ya Kindali. Hivyo mtafiti anakubali kuwa ni muhimu kuendeleza utafiti kuhusu muundo wa kirai kitenzi katika lugha za Kibantu.

ivyo basi, ili kuziba pengo hilo utafiti huu ulilenga kuongeza mchango huo kwa kuchunguza “**muundo wa kirai kitenzi katika lugha ya Kindali**”

## **2.6 Kiunzi cha nadharia**

Nadharia ni mawazo, dhana au mawazo yanayotolewa kuelezea hali fulani yaani chanzo chake, muundo wake, utenda kazi wake na mwingiliano wake wa ndani na nje (Wamitila, 2003:22). Utafiti huu umeongozwa na nadharia ya Sarufi miundo virai na dhana yake maarufu ya ndani ya kirai inayojulikana kama nadharia ya x-baa.

### **2.6.1 Nadharia ya Sarufi Miundo virai**

Kwamujibu wa Massamba (2001) anaeleza kuwa sarufi miundo virai ni mkabala wa kuchambua lugha kwa kuigawa sentensi katika virai vinavyoiunda na kisha kuvichanganua zaidi ilikufikia neno moja lililokiunda kirai. TUKI (1990) wanafafanua kuwa, sarufi miundo virai ni kitengo cha sarufi geuza maumbo zalishi, ambacho hujikita katika matumizi ya sheria chache kuzalisha sentensi nyingi zisizo na kikomo, ambazo zina usarufi na hata zile ambazo hazijawahi kutungwa. Sheria zinazotumiwa katika sarufi miundo virai si elekezi kama zile za sarufi mapokeo bali huonesha na kufafanua viambajengo vya sentensi. Sheria hizi husaidia katika kudokeza maana ya sentensi. Sheria miundo virai hujikita katika uandikaji upya wa sheria za sarufi ambazo hudhihirisha nafasi ya uamilifu wa viambajengo vya sentensi, kuanzia kiambajengo kikubwa (sentensi) hadi kiambajengo kidogo (mofu). Riro (2012) anaeleza kuwa sarufi miundo virai ni kitengo cha sarufi geuza maumbo zalishi ambacho hujikita katika matumizi ya sheria chache kuzalisha sentensi nyingi zisizo na kikomo, ambazo zina usarufi na hata zile ambazo hazijawahi kutungwa. Sheria zinazo tumiwa katika sarufi miundo virai si elekezi kama zile za sarufi

mapokeo bali huonyesha na kufafanua viambajengo vya sentensi. Sheria hizi husaidia katika kutokeza maana ya sentensi. Sheria miundo virai hujikita katika uandikaji upya wa sentensi za sarufi ambazo hudhihirisha nafasi na uamilifu wa viambajengo vya sentensi, kuanzia kiambajengo kikubwa (sentensi) hadi kiambajengo kidogo (mofu). Kwa mfano;

Mtoto mkorofi alivunja kijiko kizuri.

1. S  $\longrightarrow$  KN+KT
2. KN1  $\longrightarrow$  N1+KV1
3. KT  $\longrightarrow$  T+KN2
4. KN2  $\longrightarrow$  N2+KV2
5. N1  $\longrightarrow$  M-toto
6. N2  $\longrightarrow$  ki-jiko
7. KV1  $\longrightarrow$  m-korofi
8. KV2  $\longrightarrow$  ki-zuri
9. T  $\longrightarrow$  a-li-vunj-a

Sheria hizi zinaweza kutumiwa kuunda sentensi nyingine ama kwa kutumia maneno yaleyale kwakuyaweka katika nafasi tofauti au kwakutumia maneno mengine badala ya maneno yaliyotumiwa.

### 2.6.2 Nadharia ya x-baa

Nadharia ya x-baa ilitangulizwa na Chomsky (1970) na inashughulikia jaribio la kupata suluhisho la tatizo la sarufi miundo virai. Massamba (2004) anafafanua kuwa, nadharia ya x-baa ni nadharia ya sarufi miundo virai iliyoendelezwa baada ya ile ya



sarufi miundo virai. Hoja muhimu katika nadharia hii ni kwamba sheria zasarufi miundo virai hazina budi kudhibitiwa, na kwamba kategoria zaidi ya virai hazina budi kuongezwa. Mfano katika kategoria ya virai vitenzi kuna haja ya kuingiza kategoria nyingine ambazo ni kubwa kuliko kitenzi lakini ni ndogo kuliko kirai.

Radford (1988) anaeleza kuwa nadharia ya x-baa inazingatia ugawaji wa vipashio mbalimbali vya kileksika katika viwango tofauti katika sentensi. Ni upangaji unao baina ni kipashio kipi kina uhusiano wa ngazi moja na niki kina miliki kipi.


Leffel na Bouchard (1991) wanasema x-baa husimama kama neno kuu ambalo linaweza kuwa nomino, kitenzi, kielezi, kivumishi nakadhalika katika muundo wa kirai, x-baa husimama kama muundo kiini. Hivyo kirai cha kategoria fulani kitakuwa na neno ambalo ndicho kiini cha kirai hicho. Mfano, kirai kitenzi (KT) kiini chake kitakuwa kitenzi ambacho itachukuwa nafasi ya X katika muundo wa kirai kitakacho tumika katika utafiti huu. Vilevile kisitari juu ya X-baa humaanisha vijalizo ambavyo hulifuata neno kuu katika muundo wa kirai kistari hicho kinaweza kuwa kielezi, sentensi nakadhalika. Kiini cha kirai ndicho kinacho panga muundo wa kirai chochote kiwacho. Neekemiah (2010) akimnukuu Radford (1981) anaeleza kuwa ni vizuri kuchanganua miundo ya kisintaksia kwa kugegemeza uchanganuzi wetu kwenye mkabala wa kategoria kirai na si kwenye mkabala wa maneno. Kutokana na hali hiyo, mtafiti katika utafiti huu ametumia nadharia hii kuonesha miundo mbalimbali ya kirai kitenzi cha Kindali. Halikadhalika, nadharia imetuwezesha kuona na kubainisha vipashio vinavyoweza kutokea baada ya kitenzi katika lugha Kindali. Aidha nadharia hii imesaidia mtafiti kuona mpangilio wa vipashio hivyo katika muundo wa kirai kitenzi na hali ya kukubalika katika utokeaji wa vipashio

kulingana na miundo mbalimbali ya kirai kitenzi inayojitokeza katika lugha ya Kindali.

Pamoja na hayo, nadharia hii ina njia mbili kuu za kuchanganua miundo ya kisintaksia ambayo ni matawi na mabano. Katika utafiti huu miundo ya kirai kitenzi imechanganuliwa kwa kutumia matawi ya kisintaksia, kwa kuwa, matawi hayo huonesha uhusiano wa moja kwa moja wa vipashio vinavyounda kirai. Kwa kawaida matawi haya huchomoza kutoka kwenye viambajengo. Kila kifundo katika tawi huwa kiambajengo kilichomo katika muundo wa kirai au sentensi. Kifundo kinachokaa juu katika mti wa kisintaksia hujulikana kama kifundo cha juu na ndicho kiamba jengo kikubwa. Kifundo hiki ndicho hutawalia vifundo vya chini ambavyo hubeba viambajengo vidogo. Katika matawi haya vifundo vya chini hupangana kisafu kuonesha kipashio kipi hutangulia kingine. Vifundo vilivyo pangana kisafu hujulikana kama vifundo dada ambavyo hutawaliwa moja kwa moja na kifundo cha juu (Fromkin, 2000). Kwamfano, ikiwa KN kitakuwa kifundo cha juu na kitawalia ni N na V ambavyo vitakuwa ni vifundo vya chini na pia ni viamba jengo vidogo. taratibu hizi za mpangilio wa vifundo vya viambajengo kiwima na kisafu zimeibua dhana mbili muhimu zinazojulikana kama “utawalia” na “utangulizani”. Utawalia huhusu uhusiano wa kifundo cha juu nacha chini yake. Uhusiano huo unaoneshwa kwamistari, huonesha kuwa kifundo cha chini ni kiamba jengo cha kifundo cha juu. Kifundo cha juu huweza kutawalia kifundo cha chini kimoja, viwili, vitatu au zaidi.

Utangulizani kwa upande mwingine huonesha uhusiano wa vifundo kisafu. Hapa vifundo vya chini vinavyotawaliwa moja kwa moja na kifundo cha juu huitwa

dada. Vifundo dada hujipanga katika daraja sawa kisafu na huwa jirani pale vinapo husika vifundo viwili vinavyotawaliwa moja kwa moja na vifundo vya juu (Fromkin, 2000). Hebu tuangalie uchanganuzi wa muundo wa kirai kitenzi katika kiswahili sanifu kwa njia ya matawi ya kisintaksia hapa chini ili tuweze kuona hali tuliyo ieleza, mfano kirai kitenzi; Anacheza mpira.



Njia nyingine inayotumika kuchanganua muundo wa kirai ni ile ya mabano. Njia hii huhusu matumizi ya mabano mraba ambayo hutenganisha vipashio vyote vilivyomo katika kiambajengo kwakutumia mabano hayo. Kiambajengo huvidhibiti viambajengo vidogo vinavyounda kirai au sentensi. Hebu tuangalie mfano ufuatao ili tuone uchanganuzi wa muundo wa kirai kitenzi kwa njia ya mabano kutoka kiswahili sanifu hapa chini.

*Alimwadhibu mwanafunzi*

[KT[ T *alimwadhibu*][N *mwanafunzi*]].

Tukilinganisha njia hizo mbili za kuchanganua muundo wa kirai kitenzi tunaona kuwa njia ya matawi ya kisintaksia ni nzuri katika kuchanganua miundo ya viambajengo katika lugha ya Kindali kwa kutawaliana na kutangulizana. Njia hii inaonekana kuwa ni nzuri zaidi kwani imetumiwa na Massamba na wenzake (2001) kuchanganua miundo ya virai katika kiswahili sanifu. Hivyo, nadharia hii ya sarufi miundo virai kwakutumia kifaa tumizi cha x-baa bila ya shaka imekubaliana na utafiti huu

kwasababu mtafiti alichunguza vijenzi vya elementi vya muundo wa kirai kitenzi katika lugha ya Kindali.

## **2.7 Hitimisho**

Sura hii imejadili mapitio ya kazi tangulizi na kiunzi cha nadharia. Mwanzo kabisa imeelezea mapitio kuhusu kirai kitenzi, tafiti zilizofanywa na wataalamu kuhusu lugha ya Kindali na muundo wa kirai kitenzi cha lugha za Kibantu. Pia imeainisha nadharia ya sarufi miundo virai iliyoasisiwa na Noam Chomsky ambayo ni nadharia ya x-baa iliyoongoza utafiti huu ili kuweza kubainisha kiini cha kirai kitenzi cha lugha ya Kindali.

## **SURA YA TATU**

### **MBINU ZA UTAFITI**

#### **3.1 Utanigulizi**

Sura hii imeonyesha mbinu zilizotumika katika kukusanya data za utafiti huu. Tumefafanua eneo la utafiti, mbinu za ukusanyaji data, vifaa vya kukusanyia data, sampuli na usampulishaji, mkabala uliotumika kuchambua data katika utafiti huu, maadili ya utafiti na changamoto ambazo zimeweza kujitokeza wakati wa ukusanyaji wa data.

#### **3.2 Eneo la utafiti**

Polit na Hungler (1999) wanaeleza kuwa eneo la utafiti ni mahali ambapo data za utafiti zinakusanywa. Utafiti huu umefanyika Mkoa wa Songwe katika wilaya ya Ileje kata ya Kafule katika kijiji cha Isoko, Kafule na Kapelekesi. Wilaya ya Ileje ilichaguliwa kwasababu ni eneo ambalo linawazungumzaji wengi wa lugha ya Kindali.

#### **3.3 Mbinu za ukusanyaji data**

Adam na Kamzora (2008) wanaeleza kuwa data ni vielelezo vinavyokubalika ambavyo vinathibitisha ukweli wa matokeo. Data za msingi kama anavyoeleza Kothari (2004) ni zile data za awali ambazo hukusanywa kwa mara ya kwanza uwandani. Data za utafiti huu zilikusanywa uwandani katika sehemu zilizoteuliwa katika utafiti huu. Data hizo ndizo zilizojibu maswali ya utafiti. Data hizo zilinukuliwa kwenye madaftari na shajara. Kothari (1990) anaifafanua dhana ya ukusanyaji wa data kama zoezi la awali katika utafiti ambao humwezesha mtafiti kupata taarifa alizokusudia ili kumfikisha kwenye malengo yake ya utafiti.

Anasisitiza kuwa hatua ya uwasilishaji na uchanganuzi wa data haiwezi kufanyika kabla ya hatua hii ya ukusanyaji wa data. Utafiti huu ulitumia mbinu ya hojaji katika ukusanyaji wa data. Mbinu hii ilitumika ili kukamilisha na kutoa matokeo ya utafiti yaliyohitajika.

### **3.3.1 Mbinu ya hojaji**

Hojaji ni mbinu ambayo hutumika kukusanya data ambapo mtafiti huandika maswali na kuwapa watoa taarifa ili wayajibu na kumrudishia (Kothari, 2004). Kwamaelezo ya Walliman (2011) anaeleza kuwa, maswali ya hojaji yako ya aina mbili. Aina ya kwanza ni maswali funge ambayo hutoa fursa kwa watafitiwa kuchagua jawabu. Faida ya aina hii ni kwamba ni rahisi kujibu na kuchanganua, pia inasaidia kupata majibu mahsusi na huepusha upendeleo. Hata hivyo aina hii ya hojaji ina mapungufu yake ambayo ni pamoja na kutokumpa mtoa taarifa fursa ya kujieleza na kufafanua majibu. Aina ya pili ya maswali ya hojaji ni maswali yasiyofunge, ambayo hutoa fursa au uhuru kwa watoa taarifa kueleza wanachokijua, pia husaidia kupata taarifa nyingi zaidi. Hata hivyo njia hii pia ina mapungufu yake ambayo ni; kumpa ugumu mtafiti kubaini majibu sahihi ya maswali yaliyo ulizwa kutokana na maelezo ya watoa taarifa kuwa mengi. Mbinu ya hojaji iliyotumika katika utafiti huu imejumuisha aina zote mbili za maswali, yaani maswali funge na yasiyofunge ili kuepusha mapungufu yatakayoweza kutokea katika mbinu hizi mbili, ikizingatiwa kila moja inapungufu yake. Hivyo mbinu hizi mbili zilitumika kwa pamoja kila moja ilisaidia kuziba mapungufu ya nyingine. Mtafiti aliwapatia hojaji hizo watoa taarifa na kuwataka wabadilishe sentensi kutoka Kiswahili sanifu na kuwa katika

lugha ya Kindali. Pia mtafiti alijaza hojaji hizo kwa wale wasio jua kusoma na kuandika na wanaojua kusoma na kuandika walijaza wenyewe.

Katika utafiti huu mbinu ya hojaji ilionekana kuwa na faida kwani; iliwezesha kukusanya data katika kundi kubwa la watoa taarifa kwa muda mfupi sana. Pia, njia hii ni rahisi katika kukusanya na kuchanganua data.

Hii ilisaidia kupata taarifa sahihi kutoka kwa walengwa ambao ni wazawa na wazungumzaji wa lugha ya Kindali.

### **3.4 Vifaa vya kukusanyia data**

Kothari (2004) anaeleza kuwa, vifaa vya utafiti ni vyombo ambavyo mtafiti huvitumia katika ukusanyaji wa data. Katika utafiti huu mtafiti alitumia vifaa kama vile kalamu, karatasi, na shajara ambavyo vilitumika katika kuandika data mbalimbali zilizopatikana katika utafiti pamoja na kompyuta katika utayarishaji wa data za utafiti.

### **3.5 Sampuli**

Kothari (2009) anafafanua kuwa, sampuli ni sehemu ndogo ya populesheni kuu ambayo huteuliwa na mtafiti ili itumike katika utafiti wake. Kwakuwa si rahisi mtafiti kuwahoji watu wote wanaozungumza lugha ya Kindali ililazimika kufanya uteuzi wa sampuli ili kupata kundi dogo la wazungumzaji wa lugha ya Kindali katika Wilaya ya Ileje kata ya Kafule. Utafiti huu umehusisha wazungumzaji wa Kindali thelathini (30) wa kati ya miaka hamsini (50) na sabini (70). Mtafiti alichagua watafitiwa hawa kwasababu wao ndio wenye umilisi mkubwa wa lugha ya kindali.

Pia mtafiti ametumia sampuli ndogo ya watafitiwa thelathini kwasababu wanazungumza lugha moja, na kwakuwa mtafiti alikuwa anatafuta muundo wa lugha na si mawazo ya watu kwahiyo sampuli ndogo hiyo ilijitosheleza kabisa.

### **3.6 Usampulishaji**

Usampulishaji ni mchakato wa uteuzi wa wahusika wachache kutoka katika populesheni kubwa. Ni mchakato wa kuteua idadi fulani ya watu au vitu kutoka kwenye jamii panapofanyika utafiti kwa maana kwamba vitu au watu walioteuliwa watakuwa na sifa zitakazowakilisha jamii nzima inayofanyiwa utafiti (Orodho na Kombo, 2002). Naye Kothari (2004) anaeleza kuwa usampulishaji ni mpango wa kuchagua sampuli maalumu kutoka katika kundi kubwa. Pia Trochim (2006) anafafanua kwamba usampulishaji ni mchakato wa kuteua watafitiwa kutoka katika kundi kubwa la watafitiwa kwa ajili ya kutoa taarifa ambazo mtafiti huzitumia katika kutoa mahitimisho ya jumla yanayowakilisha kundi kubwa la watafitiwa wake. Katika utafiti huu mtafiti alitumia sampuli lengwa. Sampuli lengwa inahusu uteuaji wa sampuli unaofanywa na mtafiti kutoka kwenye kundi kubwa na maranyingi hufanywa kwa kuzingatia uelewa alionao mtafiti kuhusu mada husika (Msabila na Nanaila, 2013). Naye Bryman (2004) anabainisha kuwa kundi lengwa ni jumla ya watu wote ambao huhusishwa katika utafiti. Usampulishaji wa kundi lengwa umetumika ili kumsaidia mtafiti kupata sampuli katika uwakilishi. Katika aina hii ya usampulishaji, walengwa waliohusika katika utafiti huu ni wazee thelathini (30) ambao walichaguliwa kwa kuzingatia kigezo cha umri kuanzia miaka hamsini (50) mpaka sabini (70) ambao walitakiwa kubadilisha sentensi za Kiswahili kuwa Kindali. Idadi hii ya watafitiwa iliteuliwa kwasababu ni idadi inayotosheleza kutoa



matokeo yanayoaminika kutokana na uteuzi sahihi wa watoa taarifa. Pia mtafiti alichagua sampuli hii kutokana na muda alionao wa kukamilisha utafiti huu kwa wakati. Sababu ya kuchagua wazee hao ni kwamba ndio hasa watumiaji na waenzi wa lugha ya Kindali kuliko vijana. Pia mtafiti hakujali jinsia katika uteuzi wa watafitiwa kwasababu jinsia haina umuhimu wowote katika muundo wa lugha.

### **3.7 Mkabala wa uchambuzi wa data za utafiti**

Utafiti huu umebainisha, kuainisha na kuchanganua virai vitenzi (KT) vya Kindali. Ilikufikia malengo ya utafiti huu mtafiti ametumia mkabala wa kimaelezo. Huu ni mkabala unaotumia maelezo kuelezea jinsi watu wanavyofikiria na kuhisi kuhusu kitu au jambo fulani (Kothari, 1990). Mkabala huu wa uchanganuzi ulipendekezwa kwasababu data zilizokusanywa zilikuwa katika hali ya maelezo. Mkabala huu wa kimaelezo ni mzuri kutumia pale unapokusanya taarifa kuhusu mawazo ya watu mitazamo yao, tabia zao na masuala ya kijamii. Mkabala wa kimaelezo ulitumika zaidi katika ubainishaji wa muundo wa kirai kitenzi cha Kindali, uainishaji wa muundo huo wa kirai kitenzi na uchanganuzi wa kirai kitenzi kwa kutumia nadharia ya sarufi miundo virai.

### **3.8 Maadili ya utafiti**

Ili kufanikisha utafiti huu, nilazima mtafitiwa aelezwe maadili ya utafiti ili aweze kutoa taarifa za kweli na uhakika. Aeker (2002) kama alivyonyukuliwa na Adamu na Kamzora (2008) wametaja maadili ya utafiti kuwa ni pamoja na haki ya kuwa na usiri yaani mtafiti hatatoa siri za watoa taarifa. Vilevile mtafiti ataeleza haki ya watoa taarifa kuhakikishiwa usalama wao, haki ya kujua madhumuni ya utafiti, haki ya kupata matokeo ya utafiti, haki ya kujibu swali walilopenda kujibu na haki ya

kukataa kushiriki kwenye utafiti. Mtafiti alitambua haki zote hizi na kuzitekeleza. Watoa taarifa walijibu maswali waliyopenda kujibu. Tatizo lolote lililotokea lilikuwa juu ya mtafiti mwenyewe.

### **3.9 Changamoto zilizojitokeza wakati wa ukusanyaji wa data**

Katika mchakato wa ukusanyaji data kwa kutumia mbinu ya hojaji, mtafiti alikutana na changamoto mbalimbali. Changamoto ambazo zilijitokeza ni pamoja na baadhi ya watoa taarifa kukataa kutoa baadhi ya taarifa kwakudhani kuwa mtafiti atafaidika na kazi hiyo. Hivyo basi, ili kutatua tatizo hilo, mtafiti aliwaonesha watafitiwa kitambulisho chake cha uanafunzi, kibali cha kufanya utafiti na pia aliwaelimisha watoa taarifa wake kuwa utafiti wake ni wakitaaluma na hauhusiani na masuala ya kibiashara. Pamoja na changamoto zote zilizojitokeza katika mchakato wa ukusanyaji wa data bado hazikuaathiri upatikanaji wa data za kutosha kutoka kwa watoa taarifa. Hivyo basi, mtafiti aliridhika na data zilizokusanywa kwani zilikiidhi malengo ya utafiti.

### **3.10 Hitimisho**

Sura hii kwa ujumla imeeleza mbinu za utafiti zilizotumika kupata data, eneo la utafiti, sampuli lengwa na mbinu iliyotumika kuwasilisha data zilizokusanywa kutoka uwandani. Mtafiti aliridhika na data alizokusanya uwandani kwa sababu zilikiidhi malengo ya utafiti. Kwa hiyo data zote zilizokusanywa zimewasilishwa kwa upana katika sura ya nne.

## SURA YA NNE

### UWASILISHAJI NA UCHAMBUZI WA DATA

#### 4.1 Utangulizi

Sura hii inawasilisha data zilizokusanywa katika eneo la utafiti. Utafiti huu umetumia njia ya hojaji kukusanya taarifa kwa wazungumzaji wa lugha ya Kindali. Mtafiti amekusanya sentensi arobaini na nne (44) ambazo zilipatikana kwa Watoa taarifa. Sentensi za lugha ya Kindali ziliorodheshwa nakufanyiwa uchambuzi. Hojaji ziliandikwa na kuchambuliwa ili kurahisisha kujibu maswali matatu ya utafiti huu kwa dhamira ya kufikia kwenye lengo kuu na malengo mahususi ya utafiti. Hivyo, uchambuzi wa taarifa za utafiti huu umefanywa kwa kuangalia mambo matatu. Kwanza kubainisha vipashio vinavyounda kirai kitenzi katika lugha ya Kindali, pili kuelezea mpangilio wa muundo wa kirai kitenzi, na tatu kujadili dhima za kisarufi za kirai kitenzi cha lugha ya Kindali.

#### 4.2 Muundo wa kirai kitenzi katika lugha ya Kindali


Lengo la kwanza la utafiti huu lilikuwa kubainisha vipashio vinavyounda kirai kitenzi katika lugha ya Kindali. Katika sehemu ifuatayo mtafiti anawasilisha data zinazoonisha miundo ya aina mbalimbali ya kirai kitenzi ilivyobainishwa katika lugha ya Kindali.

##### 4.2.1 Kitenzi peke yake (KT → T)

Katika lugha ya Kindali kuna kirai kitenzi ambacho kimeundwa na kitenzi pekee. Kirai hiki ni kile ambacho kimuundo hakihitaji kufuatiwa na vipashio vingine ili kukamilisha maana. Katika muundo huu wa kirai kitenzi, kitenzi kinachojitokeza si

elekezi kwa kuwa hakihitaji kufuatiwa na nomino au kielezi. Mifano ya kirai kitenzi chenye kitenzi peke yake kilivyotolewa na watoa taarifa katika utafiti huu ni kama:

- i. Afika(Amewasili)



Mchoro huo hapo juu ni muundo wa kirai kitenzi cha kitenzi pekee

Virai vitenzi vingine vyenye muundo huo ni kama katika sentensi zifuatazo:

- ii. Umama *aghaluka* (Mama amerudi)  
 iii. Ugwasukulu *abhuka* (Mwanafunzi ameondoka)  
 iv. *Bhakapona* (walipona)

Katika sentensi za hapo juu maneno yaliyoandikwa kwa hati ya mlazo yaani *aghaluka*, *abhuka*, na *bhakapona* ni kirai kitenzi katika lugha ya Kindali kinachoundwa na kitenzi pekee.

#### 4.2.2 Kitenzi na nomino moja (KT → T+N)

Muundo mwingine wa kirai kitenzi cha lugha ya Kindali ni kitenzi na nomino moja. Muundo huu umeundwa kutokana na kitenzi na nomino moja ambapo nomino hizo zinaweza kuwa majina ya watu, wanyama au vitu. Mifano ya muundo huu wa kirai kitenzi cha lugha ya Kindali ambayo imetajwa na watoa taarifa ni pamoja na:


*Ashimba ukarata* (Ameandika barua)

*Ujuliana ghwe mwana* (Juliana ni mtoto)

*Bhula ifilato* (Wamenunua viatu)

Katika mifano ya hapo juu maneno yaliyoandikwa kwa hati ya mlazo (*Ashimba ukarata, ghwe mwana, na bhula ifilato*) ni kirai kitenzi katika lugha ya Kindali kinachoundwa na kitenzi na nomino moja.

Ufuatao ni mfano wa uchanganuzi wa kirai kitenzi katika lugha ya Kindali chenye kitenzi na nomino moja:



Kirai kilichooneshwa hapo juu kwenye mchoro kinaonekana kuundwa na kitenzi na kirai nomino chenye nomino moja. Vipashio hivyo vinavyounda kirai kitenzi chenye kitenzi na nomino moja vina uhusiano wa utawalia na utangulizani. Katika uhusiano huo, kirai kitenzi kinatawala kitenzi na nomino wakati kitenzi kinaitangulia nomino.

#### 4.2.3 Kitenzi na nomino mbili ( $KT \rightarrow T+N+N$ )

Kirai kitenzi huundwa na kitenzi na nomino mbili. Nomino hizo ndizo zinazoleta ukamilifu wa maana husika katika tungo. Katika aina hii ya muundo, nomino mbili hukitwa katika kitenzi kimoja.

Mifano ya kirai kitenzi hiki ni:

*Amupa umwana ifyakulya* (Amempa mtoto chakula)


Urehema *amupa umwana ishimbilo* (Rehema amempa mtoto kalamu)

*Twamwima ugwasukulu idaftari* (Tumemnyima mwanafunzi daftari)

Katika mifano ya hapo juu maneno yaliyoandikwa kwa hati ya mlazo ni muundo wa kirai kitenzi kinachoundwa na kitenzi na nomino mbili nayo ni; *Amupa umwana ifyakulya*, *Amupa umwana ishimbilo*, *Twamwima umwasukulu idaftari*

Mchoro ufuatao unatoa ufafanuzi wa kirai kitenzi chenye kitenzi na nomino mbili:

Amupa umwana ifindu



Katika mchoro huo hapo juu unadhihirisha kuwa kirai kitenzi kinaundwa na kitenzi kimoja pamoja na kirai nomino kilichobeba nomino mbili.

#### 4.2.4 Kitenzi na kitenzi (KT → TS+T)

Kirai kitenzi cha aina hii kina muundo wa kitenzi kisaidizi (TS) kimoja na kitenzi kikuu (T) kimoja ambapo kitenzi kikuu hutanguliwa na kitenzi kisaidizi. Muundo wa vitenzi vya aina hii, vitenzi visaidizi vinaandamana na vitenzi vikuu pale ambapo

vitenzi husika vinahusisha hali (Jerone, 2009). Vitenzi visaidizi kazi yake ni kukamilisha muundo wa kitenzi kikuu ambacho kinaandamana na kitenzi kisaidizi husika. Hata katika lugha ya Kindali hufuata mlolongo huohuo.

Mifano ya tungo yenye kirai hicho ni

*Ighanite ukughona* (Anapenda kulala)

Ujuma *akabha akubhala* (Juma alikuwa anasoma)


Une *ingalita ukughenda* (Mimi nilichoka kutembea)

Ughwe *ukabha kwimba* (Wewe ulikuwa unaimba)

Katika mifano ya hapo juu maneno yaliyoandikwa kwa hati ya mlazo; *Ighanite ukughona*, *Akabha akubhala*, *Ingalita ukughenda*, na *Ukabha kwimba* ni muundo wa kirai kitenzi katika lugha ya Kindali uliohusisha kitenzi na kitenzi.

Mfano wa mchoro wa kirai kitenzi chenye kitenzi na kitenzi ni:

*Ighanite ukughona*




Virai vilivyooneshwa hapo juu vinaonekana kuundwa na kitenzi kisaidizi na kitenzi kikuu ambapo kitenzi kikuu hutanguliwa na kitenzi kisaidizi lakini kitenzi kisaidizi hakiwezi kufanya kazi kikiwa peke yake.


#### 4.2.5 Kitenzi na nomino na kitenzi (KT $\rightarrow$ T+N+T)

Muundo wa kirai hiki unaonesha kuwa kitenzi kinafuatiwa na nomino halafu na kitenzi tena. Kutokana na data za utafiti huu, katika lugha ya Kindali kirai chenye muundo huu kinaonekana kama ifuatavyo:

*Twamusumite umumanyishi alumbilile* (tulimwomba mwalimu ahubiri)



*Tukubhalonda abhalongoshi bhitumaghe* (Tunawataka viongozi kuwajibika)





Mfano mwingine ni;

*Amumanyishishe umwana ukwoghela* (alimfundisha mtoto kuogelea)

Virai vilivyooneshwa hapo juu kwenye michoro vinaonekana kuundwa na kitenzi, nomino pamoja na kitenzi. Vipashio hivyo vinavyounda kirai kitenzi chenye kitenzi na nomino na kitenzi vinauhusiano wa utawalia na utangulizani.

#### **4.2.6 Kitenzi na kivumishi (KT → T+V)**

Aina hii ya muundo wa kirai kitenzi ni kwamba huwa kunakuwa na kitenzi kishirikishi ambacho kinafuatiwa na kivumishi. Kirai hiki hakiwezi kuwa na kitenzi kikuu halafu kikafuatwa na kivumishi. Mtafiti anaonesha hapa chini jinsi virai hivyo vinavyojitokeza katika lugha ya Kindali.

*Agha ghata makomu* (haya si mema)


*Icho chali chibhisi* (hicho kilikuwa kibichi)

*Abho abhana bha jhanja* (hao watoto ni wajanja)

Katika mifano ya hapo juu maneno yaliyoandikwa kwa hati ya mlazo; *ghata makomu, chali chibhisi, na bha jhanja* ni muundo wa kirai kitenzi chenye kitenzi na kivumishi.

Mfano wa kitenzi chenye kitenzi na kivumishi katika mchoro ni kama ifuatavyo:

Agha ghata makomu



Katika mchoro huo hapo juu unaonesha jinsi kirai kitenzi kilivyoundwa na kitenzi na kivumishi.

#### 4.2.7 Kitenzi na kielezi (kirai kielezi) (KT → T+KE)

Data za utafiti huu zinabainisha kuwa umbo la kirai kitenzi cha Kindali lina kitenzi kikifuatiwa na kielezi. Maranyingine badala ya kuwa na kielezi kimoja kunaweza kukawa na vielezi viwili (kirai kielezi).

Mifano ya tungo yenye kirai hicho katika lugha ya Kindali ni hii ifuatayo:

Umwoto *ghwakite ngani* (Moto umewaka sana)

Ubhabha *akabha kwishamba* (Baba alikuwa shambani)


Bhoshi *bhabhukite pangelo ngani* (Wote waliondoka asubuhi sana )

Umuhesha *abhuka umusughu pangelo* (Mgeni ameondoka leo asubuhi)


Katika mifano ya hapo juu maneno yaliyoandikwa kwa hati ya mlazo yanabainisha kirai kitenzi chenye muundo wa kitenzi na kielezi nao ni; *Ghwakite ngani*, *Akabha kwishamba bhabhukite pangelo ngani*, *Abhuka umusughu pangelo*.

Mifano ya kirai kitenzi chenye muundo wa kitenzi na kielezi katika mchoro:

Umwoto *ghwakite ngani*



Bhoshi *bhabhukite pangelo ngani* *KT*




Virai vitenzi vilivyooneshwa hapo juu kwenye mchoro vinaonekana kuundwa na kitenzi na kielezi kimoja au kitenzi na vielezi viwili.

#### 4.2.8 *Kitenzi na kirai kihusishi* ( $KT \rightarrow T+KH$ )

Kirai kihusishi ni kikundi cha maneno ambacho neno kuu huwa ni kihusishi. Pia katika muundo wa kirai kitenzi kuna muundo wa kitenzi na kihusishi. Data katika utafiti huu zinadhihirisha kuwa kirai kitenzi chenye muundo huu kina kitenzi, kihusishi na kirai nomino. Muundo huu unajidhihirisha katika mfano ufuatao;

Amwile ku lyojho



Katika mchoro huo hapo juu unaonesha kuwa kirai kitenzi kimeundwa na kitenzi na kirai kihusishi

Mifano mingine ya kirai kitenzi chenye kitenzi na kirai kihusishi ni:

Ubhabha ghwao *eghite imbene kwa bhabha* (Baba yao alileta mbuzi kwa baba)

Ifyakulya *fili pa mesa* (chakula kiko kwenye meza)

Injoka *jhingile mukati mu bhwina* (Nyoka aliingia ndani ya shimo)


Sehemu iliyoandikwa kwa hati ya mlazo ndiyo kirai kitenzi chenye muundo wa kitenzi na kirai kihusishi.

#### 4.2.9 Kitenzi na sentensi (KT → T+S)

Aina hii ya muundo wa kirai kitenzi, kishazi tegemezi hukitwa kwenye kitenzi. Kwa hiyo, kirai hicho kinategemea kirai nomino (KN) ilikuwasilisha maana iliyokamili.

Mfano ufuatao unadhihirisha muundo huu katika lugha ya Kindali.

Umughanga *amtibite umubhine jhujhoabhinite majholo pabhushiku* (Daktari alimtibu mgojwa aliyeugua jana usiku)



Mchoro huo hapo juu unaonesha muundo wa kirai kitenzi ambao unaundwa na kitenzi pamoja na sentensi.

Mifano mingine ya muundo huu ni:

Umuputi *amwiputile umwumini jhujhoaghwile majholo pangelo* (Mchungaji alimwombea muumini aliyeanguka jana asubuhi)

Umwalimu *amuchapite umwasukulu jhujhoibhite ichitabhu majholo* (Mwalimu alimchapa mwanafunzi aliyeiba kitabu jana)

Maneno yaliyokwenye hati ya mlazo ni kirai kitenzi chenye muundo wa kitenzi na sentensi.

Kwa mujibu wa data zilizowasilishwa hapo juu muundo wa kirai kitenzi cha lugha ya Kindali hutawaliwa na kitenzi ambacho huwa ndicho kiini cha kirai kitenzi. Vipashio vya kirai kitenzi huja baada ya kitenzi

### 4.3 Kuchanganua mpangilio wa vipengele katika kirai kitenzi

Lengo la pili la utafiti huu linahusu mpangilio wa vipengele vya muundo wa kirai kitenzi katika lugha ya Kindali. Dhana hii inahusu virai vitenzi vyenye muundo unaohusisha kitenzi, nomino, kivumishi, kielezi na sentensi.

Data zifuatazo zinaonesha virai vitenzi mbalimbali vya lugha ya Kindali vinavyoundwa kutokana na kitenzi, nomino, kivumishi, kielezi na sentensi, kama inavyooneshwa hapa chini.

#### 4.3.1 Kirai kitenzi cha kitenzi peke yake

Kwa mujibu wa data za utafiti huu, mtafiti amegundua kuwa katika kirai kitenzi cha lugha ya Kindali chenye muundo wa kitenzi peke yake, mpangilio wake huwa ni kitenzi kimoja tu kama inavyoonekana katika mifano ifuatayo:

#### Jedwali Na.4.1 Kirai kitenzi cha kitenzi peke yake.

Afika (Amewasili)


Kindali	Afika
Mpangilio	T

#### Jedwali Na. 4.2 kirai kitenzi cha kitenzi pekee.

Umama aghaluka (Mama amerudi)

Kindali	Umama	aghaluka
Mpangilio	N	T

Uchanganuzi wa kirai kitenzi cha kitenzi pekee kina muonekano ufuatao katika mpangilio wake.



Katika mchoro huo hapo juu unaonesha kuwa katika kirai kitenzi chenye kitenzi pekee huwa na mpangilio wa kitenzi (T) peke yake

#### **/n4.3.2 Kirai kitenzi cha kitenzi na nomino moja.**

Aina h0069i kirai kitenzi kinaundwa na nomino moja. Uchanganuzi ufuatao unaonesha mpangilio wa mfuatano wa vipengele vinavyounda kirai kitenzi cha lugha ya Kindali. Data zifuatazo zinaonesha mpangilio wa nomino katika kirai kitenzi.

#### **Jedwali Na.4.3 kirai kitenzi cha kitenzi na nomino moja**

Ashimba ukarata (Ameandika barua)

Kindali	Ashimba	ukarata
Mpangilio	T	N

Bhula ifilato (Wamenunua viatu)

#### **Jedwali Na. 4.4 kirai kitenzi cha kitenzi na nomino moja**

Kindali	Bhula	ifilato
Mpangilio	T	N

Mpangilio wa muundo wa kirai kitenzi chenye kitenzi na nomino ni T+N

**Jedwali Na. 4.5 kirai kitenzi cha kitenzi na nomino moja**


Ujuliana ghwe mwana (Juliana ni mtoto)

Kindali	Ujuliana	ghwe	mwana
Mpangilio	N	T	N

Kwamujibu wa data zilizowasilishwa katika jedwali namba 4.5 mpangilio wa vipashio vya muundo wa kirai kitenzi chenye kitenzi na nomino moja kinakuwa na mpangilio ufuatao: T+N au t+N

Uchanganuzi wa kirai kitenzi cha kitenzi na nomino

Ujuliana ghwe mwana



Mchoro huo hapo juu unaonesha kuwa katika kirai kitenzi chenye kitenzi na nomino moja huwa na mpangilio wa; T+N.



### 4.3.3 Kirai kitenzi cha kitenzi na nomino mbili.

Aina hii ya kirai kitenzi katika lugha ya Kindali kinaundwa na nomino mbili. Mpangilio wake ni kitenzi, nomino na nomino. Data zifuatazo zinaonesha mfuatano huo.

#### Jedwali Na 4.6 kirai kitenzi cha kitenzi na nomino mbili

Amupa umwana ifyakulya (Amempa mtoto chakula

Kindali	Amupa	umwana	ifindu
Mpangilio	T	N	N

#### Jedwali Na. 4.7 kirai kitenzi cha kitenzi na nomino mbili


Twamwima umwasukulu idaftari (Tumemnyima mwanafunzi daftari)

Kindali	Twamwima	umwasukulu	idaftari
Mpangilio	T	N	N

Kwa mujibu wa data zilizooneshwa hapo juu inaonesha kwamba katika kirai kitenzi cha lugha ya Kindali, nomino zote mbili hujitokeza baada ya kitenzi, nomino hizo hujitokeza katika mpangilio ufuatao:

T+N+N.

Uchanganuzi wa kirai kitenzi cha kitenzi na nomino mbili kina muonekano ufuatao



Mchoro huo hapo juu unaonesha kuwa katika kirai kitenzi chenye kitenzi na nomino mbili mpangilio wake huwa T+N+N

#### 4.3.4 Kirai kitenzi cha kitenzi na kitenzi

Data za utafiti huu zinadhihirisha kuwa kirai kitenzi cha lugha ya Kindali huundwa na kitenzi na kitenzi. Data zifuatazo zinaonesha mfuatano wa vipashio katika kirai kitenzi.

#### Jedwali Na.4.8 kirai kitenzi cha kitenzi na kitenzi

Ighanite ukughona (Anapenda kulala)

Kindali	Ighanite	ukughona
Mpangilio	TS	T

**Jedwali Na. 4.9 kirai kitenzi cha kitenzi na kitenzi**

Une ingalita ukughenda (Mimi nilichoka kutembea)

Kindali	Ingalita	ukughenda
Mpangilio	TS	T

**Jedwali Na. 4.10 kirai kitenzi cha kitenzi na kitenzi**


Ughwe ukabha kwimba (Wewe ulikuwa unaimba)

Kindali	Ughwe	ukabha	kwimba
Mpangilio	N	TS	T

Kwamujibu wa data zilizowasilishwa hapo juu zinaonesha kwamba katika kirai kitenzi cha lugha ya Kindali huwa kuna kuwa na mfuatano wa kitenzi na kitenzi ambapo inakuwa kitenzi kisaidizi kikifuatiwa na kitenzi kikuu na hujitokeza katika mpangilio ufuatao; TS+T.

Uchanganuzi wa kirai kitenzi cha kitenzi na kitenzi kina muonekano ufuatao:

Une ingalita ukughenda



Uchanganuzi katika mchoro huo hapo juu unaonesha kuwa katika kirai kitenzi chenye kitenzi na kitenzi huwa na mpangilio wa TS+T.

#### **4.3.5 Kirai kitenzi cha kitenzi na nomino na kitenzi**

Kirai kitenzi cha aina hii huundwa na kitenzi na nomino na kitenzi. Mpangilio wake ni kitenzi nomino na kitenzi. Data zifuatazo zinaonesha mfuatano wa kitenzi nomino na kitenzi.

##### **Jedwali Na. 4.11 kirai kitenzi cha kitenzi na nomino na kitenzi**

Twamusumite umwalimu alumbilile (Tulimwomba mwalimu ahubiri)

Kindali	Twamusumite	umwalimu	alumbilile
Mpangilio	T	N	T

##### **Jedwali Na. 4.12 kirai kitenzi cha kitenzi na nomino na kitenzi**


Amumanyishishe umwana ukwoghela (alimfundisha mtoto kuogelea).

Kindali	Amumanyishishe	umwana	ukwoghela
Mpangilio	T	N	T

Kwa mujibu wa data zilizowasilishwa hapo juu kirai kitenzi cha lugha ya Kindali huwa kinakuwa na mfuatano wa kitenzi na nomino na kitenzi na hujitokeza katika mpangilio ufuatao:

T+N+T

Uchanganuzi wa kirai kitenzi cha kitenzi, nomino, na kitenzi ni kama ifuatavyo:



Katika mchoro huo hapo juu unaonesha mpangilio wa kirai kitenzi chenye kitenzi nomino na kitenzi kuwa ni;T+N+N

#### 4.3.6 Kirai kitenzi cha kitenzi na kivumishi

Aina ya kirai kitenzi hiki kina muundo wa kitenzi na kivumishi, maranyingi kitenzi hicho huwa ni kitenzi kishirikishi (t). Kirai hiki cha lugha ya Kindali huwa na mfuatano wa kitenzi kishirikishi (t) na kivumishi (V). Data zifuatazo zinaonesha mfuatano kitenzi na kivumishi.

#### Jedwali Na.4.13 kirai kitenzi cha kitenzi na kivumishi

Agha ghata makomu (Haya siyo mema)

Kindali	Agha	ghata	makomu
Mpangilio	N	T	V

**Jedwali Na.4.14 kirai kitenzi cha kitenzi na kivumishi**

Icho chikabha chibhisi (Hicho kilikuwa kibichi)


Kindali	Icho	Chikabha	chibhisi
Mpangilio	N	T	V

Kwahiyo kutokana na data hizo hapo juu kirai kitenzi katika lugha ya Kindali huwa katika mpangilio ufuatao:

T+V

Uchanganuzi wa kirai kitenzi cha kitenzi na kivumishi ni kama ilivyooneshwa hapa chini:

Icho chikabha chibhisi



Mchoro huo hapo juu unaonesha mpangilio wa kirai kitenzi katika lugha ya kindali kuwa ni; T+V.

#### 4.3.7 Kirai kitenzi cha kitenzi na kielezi

Data za utafiti huu zinadhirisha kuwa kirai kitenzi cha aina hii kina muundo wa kitenzi na kielezi maranyingine huweza kuwa na vielezi viwili vinavyofuatana. Kirai kitenzi hiki cha lugha ya Kindali huwa na mfuatano wa kitenzi na kielezi au vielezi viwili. Data zifuatazo hapa chini zinaonesha mpangilio huo;

#### Jedwali Na.4.15 kirai kitenzi cha kitenzi na kielezi

Bhoshi bhabhukite pangelo ngani (Wote waliondoka asubuhi sana)

Kindali	Bhoshi	bhabhukite	Pangelo	ngani
Mpangilio	N	T	E	E


Mchoro huo hapo juu unaonesha mfuatano wa vielezi viwili.

Kutokana na data hizo hapo juu kirai kitenzi cha lugha ya Kindali huwa na mpangilio ufuatao;

T+E au T+E+E

Uchanganuzi wa kirai kitenzi cha kitenzi na vielezi viwili ni kama ifuatavyo:

Bhoshi bhabhukite pangelo ngani



Mchoro huo hapo juu unaonesha kuwa katika kirai kitenzi chenye vielezi viwili au kirai kielezi huwa na mpangilio wa;T+E+E.

#### 4.3.8 Kirai kitenzi cha kitenzi na kirai kihushi

Kirai kitenzi cha aina hii huwa na muundo wa kitenzi na kirai kihusishi. Kirai kitenzi hiki huwa na mfuatano wa kitenzi na kirai kihusishi. Data zifuatazo zinaonesha mfuatano huo:

#### Jedwali Na.4.16 kirai kitenzi cha kitenzi na kirai kihusishi

Udamasi amwile kulyojho (Damasi alijibu kwa hasira)

Kindali	Udamasi	amwile	ku lyojho
Mpangilio	N	T	KH



**Jedwali Na.4.17 kirai kitenzi cha kitenzi na kirai kihusishi**


Injoka jhingile mukati mu bhwina (Nyoka aliingia ndani ya shimo)

Kindali	Injoka	jhingile	mukati mu bhwina
Mpangilio	N	T	KH

Kwa hiyo data hizo hapo juu zinaonesha kwamba kirai kitenzi cha lugha ya Kindali huwa na mpangilio wa T+KH

Uchanganuzi wa kirai kitenzi hiki unaweza kuthibitishwa katika mchoro ufuatao:

Injoka njhingile mukati mu bhwina



Mchoro huo hapo juu unaonesha kuwa katika kirai kitenzi huwa na mpangilio wa T+KH

#### 4.3.9 Kirai kitenzi cha kitenzi na sentensi

Aina ya kirai kitenzi hiki huwa na muundo wa kitenzi na sentensi. Aina hii ni mfano wa kishazi tegemezi kinachokitwa kweye kitenzi, kwa hiyo kirai kitenzi hiki huwa na mfuatano wa kitenzi na sentensi.

Data zifuatazo zinaonesha mfuatano huo:

#### Jedwali Na.4.18 kirai kitenzi cha kitenzi na sentensi

Umughanga amutibite umubhine jhujho abhinite majholo pabhushiku (Daktari alimtibu mgonjwa aliyeugua jana usiku)

Kindali	Umughanga	amutibite	umubhine jhujho abhinite majholo pabhushiku
Mpangilio	N	T	S

#### Jedwali Na.4.19 kirai kitenzi cha kitenzi na sentensi


Umwalimu amuchapite umwasukulu jhujho ibhite ichtabhu majholo (Mwalimu alimchapa mwanafunzi aliyeiba kitabujana)

Kindali	Umwalimu	Amuchapite	umwasukulu jhujhoibhite ichtabhu majholo
Kindali	N	T	S

Kutokana na data zilizowasilishwa hapo juu cha kirai kitenzi cha lugha ya Kindali huwa na mpangilio ufuatao:

T + S.

Mchoro ufuatao unaonesha mpangilio huo;



Mchoro huo hapo juu unaonesha kuwa kirai kitenzi katika lugha ya Kindali huwa na mpangilio wa T+ S.

Kwa mujibu wa data zilizowasilishwa hapo juu vipashio vya muundo wa kirai kitenzi vinadhihirisha kuwa vipashio mbalimbali vinavyounda kirai kitenzi vinafuata utaratibu maalumu wa mfuatano. Data zote zinaonesha kwamba kirai kitenzi cha lugha ya Kindali kinatawaliwa na kitenzi ambacho ndicho huwa kiini cha kirai kitenzi. Baada ya kitenzi hufuatiwa na maneno mengine ambayo ni; nomino moja, nomino mbili, nomino na kitenzi, kivumishi, kielezi, kirai kihusishi, na sentensi ambayo huwa kishazi tegemezi kilichokitwa katika kitenzi.

#### 4.4 Kubainisha dhima za kisarufi za kirai kitenzi katika lugha ya Kindali.

Lengo la tatu la utafiti huu lilikuwa kubainisha dhima za kirai kitenzi katika lugha ya Kindali. Lengo lilikuwa kuonesha kazi zinazofanywa na kirai kitenzi katika miundo ya sentensi ya lugha ya Kindali.

Data zifuatazo zinaonesha dhima mbalimbali za kirai kitenzi katika lugha ya Kindali:

##### 4.4.1 Kirai kitenzi hutumika kama kivumishi cha kirai nomino.


Kirai kitenzi cha lugha ya Kindali kina dhima ya kuvumisha au kuelezea kuhusu kirai nomino. Data zifuatazo zinaonesha namna kirai kitenzi cha lugha ya Kindali kinavyodhihirisha dhima hiyo kisarufi:

Ujuma *indiakaghaluke pamande* (Juma atarudi Jumatatu)

Umwoto *ghwakite ngani* (Moto umewaka sana)

Katika mifano iliyooneshwa hapo juu maneno yaliyoandikwa kwa hati ya mlazo yanadhihirisha dhima ya kirai kitenzi katika lugha ya Kindali yaani, kinavyovumisha kirai nomino

Ujuma *indiakaghaluke pamande*



Katika uchanganuzi wa sentensi hiyo hapo juu kirai kitenzi”indiakaghaluke Pamande” kinaonesha jinsi kinavyovumisha kirai nomino “Ujuma”.

#### **4.4.2 Kirai kitenzi hufanya kazi kama kijalizo cha kirai nomino.**

Kirai kitenzi katika lugha ya Kindali kina dhima ya kuwa kijalizo cha kirai nomino katika sentensi. Massamba (2004), anafafanua kijalizo kama kiambajengo cha sentensi au kishazi ambacho katika sarufi mapokeo kimechukuliwa kuwa na kazi ya kukamilisha maelezo yaelekezwayo na kitenzi.


Data zilizowasilishwa hapo chini zinaonesha jinsi kirai kitenzi katika lugha ya Kindali kinavyofanya kazi ya kuwa kijalizo cha kirai nomino.

Ujuliana *ghwe mwana* (Juliana ni mtoto)

Umwene akukindagha bhwila (yeye hukimbia kila siku)

Mifano iliyooneshwa hapo juu maneno yaliyokwenye hati ya mlazo yanaonesha jinsi kirai kitenzi cha lugha ya Kindali kinavyofanya kazi ya kuwa kijalizo cha kirai nomino.

Uchanganuzi ufuatao unaonesha namna kirai kitenzi cha lugha ya Kindali kinavyofanya kazi ya kuwa kijalizocha kirai nomino



Uchanganuzi wa sentensi ulioneshwa hapo juu unaonesha jinsi kirai kitenzi kinavyofanya kazi ya kuwa kijalizo cha kirai nomino yaani kirai kitenzi” akukindagha kilalishiku” ni kijalizo cha kira nomino“Umwene

Katika sura hii mtafiti amebainisha muundo wa kira kitenzi katika lugha ya Kindali ambapo data zimeonesha kuwa kirai kitenzi cha lugha ya Kindali kina miundo ifuatao; kitenzi peke yake, kitenzi na nomino moja, kitenzi na nomino mbili, kitenzi na kitenzi, kitenzi nomino na kitenzi, kitenzi na kivumishi, kitenzi na kielezi, kitenzi na kirai khusishi na kitenzi na sentensi.

Katika sura hii, pia mtafiti amechambua mpangilio wa vipashio vinavyounda kirai kitenzi katika lugha ya Kindali.

Mpangilio wa vipengele vya kirai kitenzi cha lugha ya Kindali hutawaliwa na kitenzi ambacho hufuatiwa na maneno mengine yanayotoa ufafanuzi zaidi kuhusu kitenzi hicho.

Kwa mujibu wa data zilizowasilishwa hapo juu na uchambuzi uliofanywa, matokeo yafuatayo yamebainika kuhusu muundo wa kirai kitenzi cha lugha ya Kindali; kwanza kuhusu muundo, imebainika kuwa Kindali kina virai vitenzi vya aina zifuatazo; kirai kitenzi cha kitenzi pekee, kirai kitenzi cha kitenzi na nomino moja, kirai kitenzi chenye kitenzi na nomino mbili, kirai kitenzi chenye kitenzi na nomino na kitenzi, kirai kitenzi chenye kitenzi na kivumishi, kirai kitenzi chenye kitenzi na kielezi, kirai kitenzi chenye kitenzi na kirai kihusishi na, kirai kitenzi chenye kitenzi na sentensi.

Kuhusu dhima za kisarufi za kirai kitenzi imebainika kuwa kirai kitenzi katika lugha ya Kindali kina dhima zifuatazo kisarufi; dhima ya kwanza hufanya kazi ya kuvumisha kirai nomino, dhima ya pili hufanya kazi kama kijalizo cha kirai nomino.

#### **4.4 Hitimisho**

Katika uchambuzi uliofanyika hapo juu mtafiti ameweza kubainisha miundo mbalimbali ya kirai kitenzi cha lugha ya Kindali, kisha amechanganua mpangilio wa vipengele katika kirai kitenzi. Vilevile mtafiti alielezea dhima za kisarufi za kirai kitenzi.

## **SURA YA TANO**

### **MUHTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO YA UTAFITI**

#### **5.1 Utangulizi**

Hii ni sura ya mwisho ya ripoti ya utafiti uliochunguza muundo wa kira kitenzi katika lugha ya Kindali. Katika sura hii mtafiti ameangalia muhtasari wa utafiti, muhtasari wa matokeo ya utafiti, mapendekezo ya utafiti pamoja na hitimisho la utafiti. Malengo mahususi ya utafiti huu yalikuwa ni kubainisha miundo ya kirai kitenzi katika lugha ya Kindali, kubainisha mpangilio wa vipashio vya muundo wa kirai kitenzi katika lugha ya Kindali pamoja na kubainisha dhima za kisarufi za kirai kitenzi cha lugha ya Kindali.

#### **5.2 Muhtasari wa Utafiti**

Sura ya kwanza ilieleza kuwa watalaamu mbalimbali walifanya utafiti katika lugha ya Kindali kwa vipengele mbalimbali, lakini hakuna utafiti uliofanywa kuhusu kirai kitenzi cha lugha ya Kindali, hivyo mtafiti aliamua kulichunguza tatizo hili kiundani. Vilevile sura hii imeeleza malengo ya utafiti pamoja na maswali ya utafiti ambayo yameongoza katika ukusanyaji wa data za utafiti huu.

Malengo ya utafiti yalikuwa matatu nayo ni kuchunguza muundo wa kirai kitenzi katika lugha ya Kindali, kuchunguza mpangilio wa vipashio vya kirai kitenzi katika lugha ya Kindali na mwisho ni kubainisha dhima za kirai kitenzi katika lugha ya Kindali.

Sura ya pili imeonesha kazi tangulizi ambazo zinahusu lugha ya Kindali na zinazohusu Kiswahili sanifu. Pia kiunzi cha nadharia iliyotumika katika uchanganuzi



wa data za utafiti huu kimebainishwa. Nadharia hiyo ni nadharia ya eksibaa ambayo mwandishi wake ni Noam Chomsky.

Sura ya tatu imejadili eneo la utafiti, mkabala wa utafiti, sampuli ya utafiti, mbinu za utafiti na uteuzi wa sampuli za utafiti. Utafiti huu umefanywa katika wilaya ya Ileje ambako ndiko wazungumzaji wa lugha ya Kindali wanapatikana. Walengwa wa utafiti walikuwa ni wazee wenye umri wa kuanzia miaka hamsini (50) na sabini (70) kati ya walioteuliwa walikuwa walengwa thelathini (30) kama sampuli ya washiriki wa utafiti huu. Mwisho utafiti huu umetumia njia ya hojaji ambayo ilitolewa kwa watafitiwa ili kutoa data zilizosahihi.

Sura ya nne imehusu uchambuzi wa data za kirai kitenzi katika lugha ya Kindali. Kirai kitenzi cha lugha ya Kindali kinaundwa na kirai kitenzi chenye kitenzi pekee, kitenzi na nomino moja, kitenzi na nomino mbili, kitenzi na kitenzi, kitenzi nomino na kitenzi, kitenzi na kivumishi, kitenzi na kielezi, kitenzi na kirai kihusishi na, kitenzi na sentensi.

### **5.3 Muhtasari wa Matokeo ya Utafiti**

Utafiti huu umebainisha miundo tisa (9) ya kirai kitenzi cha lugha ya Kindali ambayo ni kirai kitenzi chenye kitenzi pekee, kitenzi na nominomoja, kitenzi na nomino mbili, kitenzi na kitenzi, kitenzi, nomino na kitenzi, kitenzi na kivumishi, kitenzi na kielezi, kitenzi na kirai kihusishi na, kitenzi na sentensi.

Vilevile, mpangilio wa vipashio vinavyounda kirai kitenzi cha lugha ya Kindali ni kirai kitenzi kubeba kitenzi ambacho ndicho huwa kiini. Baada ya kitenzi vinafuatia

vipashio vingine vinavyoambatana na kitenzi ambavyo ni nomino ambayo yaweza kuwa nomino moja au mbili, kielezi au vielezi , kirai kihusishi na, sentensi.

Pamoja na hayo, katika sentensi za Kindali kirai kitenzi kinabeba dhima za kisarufi ambapo kirai kitenzi hufanya kazi ya kuvumisha kirai nomino katika sentensi, pia hufanya kazi kama kijalizo cha kirai nomino.

#### **5.4 Mapendekezo ya Utafiti**

Utafiti huu ulichunguza muundo wa kirai kitenzi cha lugha ya Kindali, ambao umeegemea zaidi katika kuangalia vipashio vinavyoandamana na kirai kitenzi cha lugha ya Kindali. Mtafiti anapendekeza kufanyika utafiti ambao utaangalia kirai kihusishi cha lugha ya Kindali kwa kutumia nadharia ya x-baa.

#### **5.5 Hitimisho**

Utafiti huu umefafanua muundo wa kirai kitenzi cha lugha ya Kindali. Data za utafiti huu zimebainisha namna kitenzi kinavyoandamana na vipashio vingine ili kuunda kirai kitenzi. Hivyo, utafiti huu utaongeza ari kwa watafiti wengine kufanya tafiti zaidi kuhusiana na lugha ya Kindali kwa lengo la kujaza maarifa kuhusu sarufi ya lugha hiyo.

### MAREJELEO

- Adam, J. na Kamzora, F. (2008). *Research Methods for Business and social studies*. Morogoro, Tanzania: Mzumbe Book Project.
- Barongo na wenzake. (2019). *Kiswahili shule za Sekondali kitabu cha Mwanafunzi Kidato cha Tano na Sita-Lugha na Sarufi*. Dar es Salaam: TET.
- Botney, R. (1998). *Prosodically conditioned Vowel shortening in Chindali*. journals of Studies in African Linguistics. Indian University, V27, NO 1
- Botney, R and Schafer, L (2008). *A Chindali and English Dictionary with an Index to Proto-Bantu roots*. Philadelphia: American philosophical Society.
- Fromkin, V. A. (2000). *Linguistics: An Introduction to Linguistics Theory*. Black well. Publishers inc. malden, U.S.A: Massachussetts.
- John, J. na Mduda, F. (2012). *Kiswahili Kidato cha Tano na Sita*. Dar es salaam: Oxford University Press.
- Habibu, N. (2016). *Muundo wa Kirai Kitenzi katika Lugha ya Kisambaa*. Tasnifu ya shahada ya uzamili; Chuo kikuu cha Dar es Salaam. Dar es Salaam Tanzania.
- Haji, N.M. (2018). *Muundo wa kirai kitenzi katika lahaja ya Kitumbatu*. Tasnifu ya shahada ya uzamili: Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.
- Kibona, N . (2019). *The analysis of Noun phrase in Chindali*. Journal of language Teaching and Research, Vol 10, No 5, pp 906-913.

- Kihore, M.Y. na wenzake (2012). *Sarufi Maumbo Ya Kiswahili Sanifu (SAMIKISA) Sekondari na Vyujo*. Dar es Salaam: TUKI
- Kothari, C. R. (2004). *Research Methodology, Methods and Techniques* (toleo la pili). New delhi: New Age International (p) Limited Publishers.
- Kothari, C. R. (1990). *Research Methods; Methods and Techniques*. New Delh: Wiley Eastern.
- Leffel, K. na Bouchard, D. (1991). *Views on Phrase Structure*. Dordrecht, The Netherlands: Kluwer Academic Publisher.
- Masebo, H. (2007). *Verb extensions in Chindali*. MA dissertation, University of Dar es salaam.
- Masebo, J. na Nyangwine, N. (2016). *Nadharia ya lugha ya Kiswahili 1 kidato cha 5 na 6*. Dar-es-salaam: Nambari Nyangwine publishers.
- Massamba, D.P.B. na wenzake. (2001). *Sarufi Miundo ya Kiswahili Sanifu (SAMIKISA) Sekondari na Vyujo*. Dar es Salaam: TUKI.
- Massamba, D.P.B. (2004). *Kamusi ya Isimu na Falsafa ya Lugha*. Dar-es-salaam: Dar-es-salaam Univesity press.
- Massamba na wenzake (2001). *Sarufi Miundo ya Kiswahili Sanifu (SAMIKISA) Sekondari na Vyujo*. Dar es Salaam: TUKI.
- Matei, A. (2008). *Sarufi Kamili ya Kiswahili*. Nairobi: Phoenix.

- Mdee J.S. (1999). *Sarufi ya Kiswahili Sekondari na vyuo*. Dar-es-Salaam: Dar-es-Salaam University Press.
- Mgulu, S.R.(2012). *Mtaala Wa Isimu Fonetiki, Fonolojia, na Mofolojia Ya Kiswahili*. Dar es Salaam: Longhorn Publishers (T) Ltd.
- Mshani, E.(2014). *Maumbo na dhima ya uradidi wa vitenzi katika lugha ya Chindali*. Masters Dissertations. Dar es salaam university.
- Mugisa, M. J. (2011). *The Syntactic Structure of VP in Kihema* .Stellen Bosch papers in Linguistics: DRC.University of Kwazulu-Natal, Vol.40, 2011,1-19.
- Ondondo (2015). *The structure of a Kisa verb phrase*.International Journal of English/Language and linguistic Research, Vol 3.NO.5.pp 9 - 24
- Radford, A. (1981). *Transformational Syntax*. Cambridge: Cambridge University Press.
- Radford, A. (1988). *Transformational Grammar*. Cambridge. Cambridge University Press.
- Radford, A.(2004). *English Syntax: An introduction*.Cambridge:Cambridge University Press.
- Riro, S.M. (2012). *Dafina ya Lugha Isimu na Nadharia kwa Sekondari, Vyuo vya kati na Vyuo vikuu*.Mwanza: Serengeti Educational Publishers (T) Ltd.

- Swilla, I.N. (2005). *The Dyanamics of Language Maintenance among Speakers of Chindali in Mbozi District, TANZANIA*. Jounals of Asian and African Studies: University of Dar es salaam, VI, NO 70
- Swilla, I.N. (1998). *Tenses in Chindali*.Africanistische Arbeit Papier-AAP54:95-117.
- Swilla, I,N.(2000). *Names in Chindali*.Africakanistische Arbeits papiere, 63, pg. 35-61
- TUKI (1990). *Kamusi Sanifu ya Isimu ya Lugha*.Chuo Kikuu cha Dar-es-Salaam: TUKI.
- Walliman, N. (2011). *Research Methods:The Basic*.London and New York:Routledge Taylor and Francis Group.

## **VIAMBATANISHO**

**KIAMBATANISHO A:** Hojaji kwa wakazi wa Ileje.

Mimi naitwa Denis Lamson Kibona ni mwanafunzi ninayesomea shahada ya uzamili (M.A Kiswahili) katika chuokikuu huria cha Tanzania. Ninafanya utafiti kuhusiana na kirai nomio cha lugha ya Kindali ilikuweza kukamilisha shahada hii. Hojaji imeandikwa kwakusudi la kupata taarifa zitakazo kamilisha utafiti huu. Hivyo ninaomba ushirikiano wako katika kukamilisha malengo ya utafiti huu.

Tafadhali unaombwa kujibu maswali yafuatayo kwa mujibu wa uelewa wako na kwa usahihi ili usaidie kutoa matokeo yakinifu yatakayo changia maendeleo ya lugha ya Kindali. Majibu yatakayo tolewa yata kuwa siri ya mtafiti na hayata tumika kwa malengo mengine yoyote zaidi ya utafiti huu.

### **SEHEMU YA KWANZA: MAELEZO BINAFSI**

Maelekezo: Tafadhari weka tiki au maelezo mafupi pale panapohusika

1. Jinsia (i) Mke (ii) Mme (iii) nyingine
2. Kiwango cha elimu (i) hujasoma (ii) msingi (iii) sekondari (iv) chuo
3. Kijiji unachoishi.....
4. Miaka mingapi umeishi katika kijiji hiki.....

**SEHEMU YA PILI: MAELEZO KUHUSU KIRAI KITENZI**

Katika maswali yafuatayo badilisha sentensizifuatazo kuwa katika lugha ya Kindali.

1. Amewasili.....
2. Anapenda kulala.....
3. Amempa mtoto chakula.....
4. Moto umewaka sana.....
5. Tunawataka viongozi kuwajibika.....
6. Rehema amempatia mtoto Kalamu.....
7. Tulimwomba mwalimu ahubiri.....
8. Alimfundisha mtoto kuogelea.....
9. Yeye hukimbia kila siku.....
10. Tumemnyima mwanafunzi daftari.....
11. Ameandika barua.....
12. Mama amerudi.....
13. Juma alikuwa anasoma.....
14. Nyoka aliingia ndani ya shimo.....
15. Wamenunua viatu.....
16. Hamisi alitukaribisha vizuri sana.....
17. Mlinzi alitukamata tulipokuwa tunatoroka.....
18. Damasi alijibu kwa hasira.....
19. Mwalimu alimchapa mwanafunzi aliyeiba kitabu jana.....
20. Hamisi alikuwa anatafutwa.....
21. Hao watoto ni wajanja.....
22. Mwalimu yumo darasani.....



23. Juliana ni mtoto.....
24. Mwajuma ni shangazi yangu.....
25. Mwanafunzi ameondoka.....
26. Baba alikuwa shambani.....
27. Haya si mema.....
28. Wamepona.....
29. Juma atarudi Jumatatu.....
30. Wote waliondoka asubuhi sana.....
31. Daktari alimtibu mgonjwa aliyeugua jana usiku.....
32. Anakula.....
33. Mimi nilichoka kutembea.....
34. John alileta gari dogo.....
35. Hamis haji leo.....
36. Anatafuta kazi nzuri .....
37. Baba yao alileta mbuzi kwa babu.....
38. Watoto walirudi tena.....
39. Mgeni ameondoka leo asubuhi.....
40. Mchungaji alimwomba muumini aliyeugua jana asubuhi
41. Chakula kiko kwenye meza.....
42. Kulima kwake kunafurahisha.....
43. Wewe ulikuwa unaimba.....
43. Giza lilikuwa linatisha kutembea usiku .....
44. Choo kilikuwa ndani.....

**ASANTE KWA USHIRIKIANO WAKO.**

### **KIAMBATANISHO B: RATIBA YA UTAFITI**

Septemba, 2019

- Uandaaji wa pendekezo la utafiti
- Uhudhurishaji wa pendekezo la utafiti kwenye ngazi ya idara na kitivo.
- Kutafutavibali vya kuruhusu utafiti uwandani.

Oktoba, 2019

- Safari katika maeneo ya utafiti.
- Uteuzi wa saidizi katika katika shughuli ya utafiti
- Uteuzi wa wasailiwa kwa msaada wa wasaidizi.
- Kuwaandaa watafitiwa kushiriki katika utafiti.

Novemba, 2019

- Utafiti uwandani
- Mahojiano ya ana kwa ana na wasailiwa watakaoteuliwa

Disemba, 2019-Januari, 2020

- Kuchambua na kuchanganua data
- Kuandaa rasmu ya kwanza
- Kuhudhurisha rasimu ya kwanza katika ngazi ya idara
- Kuandaa tasnifu kwa kuzingatia maoni na marekebisho katika ngazi ya kitivo
- Kuwasilisha tasifu katika katika ngazi ya idara, kitivo na kurugenzi ya uzamili.

**KIAMBATANISHO C: MAKADIRIO YA BAJETI YA UTAFITI**

NAMBA	MATUMIZI	KIASI
1	Usafiri	150000
2	Chakula	140000
3	Kalamu ya wino na risasi	2000
4	Karatasi	10000
5	Kuunganisha kazi	3000
6	Kutoa kopi	10000
7	Malipo kwa wasaidizi wawili	100000
8	Jumla	480000